BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Thelathini na Mbili - Tarehe 16 Julai, 2010

(Mkutano ulianza Saa Tisa Alasiri)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge, inapofika siku ya Mheshimiwa Rais Kuhutubia Bunge hili inabidi nilitaarifu Bunge rasmi.

Sasa natoa taarifa rasmi kwamba leo tarehe 16 Julai, 2010 imempendeza mwaka huu wa 2010 Mheshimiwa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aje kulihutubia Bunge hili. Kwa ajili hiyo, nitasitisha shughuli za Bunge hadi hapo atakapokuja.

Tunamtegemea Mheshimiwa Rais kuwasili kwenye viwanja Bunge mnamo saa tisa na dakika thelathini. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi kamili alasiri; hapa katikati, kati ya saa tisa na nusu na saa kumi nitawaomba Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge na Makamishna tumpokee Mheshimiwa Rais wetu. Kama ilivyo kawaida yetu hapa Bungeni, mahali tunapokutania ni pale kwenye ngazi, mbele ya lango kuu la kuingilia katika Ukumbi huu wa Bunge. Kwa hiyo, nitawaomba sasa msimame.

(Hapa Spika alikumbushwa Hati za Mezani)

SPIKA: Kuna Hati? Leo *Secretariat* mbona mnachanganya hivyo. Basi samahani Waheshimiwa Wabunge, muendelee kuketi, nilijua ingetangulia Hati. Lakini wanasema Hati inafuata, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Taarifa ya utekelezaji wa ahadi za Serikali Bungeni kwa mwaka 2009/2010.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge. Sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo mtakapoitwa baada ya kuwasili Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

(Hapa Bunge lilisitishwa ili kumpokea Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dr. Jakaya Mrisho Kikwete)

(Bunge lilirudia)

(Hapa Maandamano ya Majaji na Makatibu Mezani yaliingia Bungeni)

MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA: Akinamama wanaweza! *(Kicheko/Makofi/Vigelegele)*

(Hapa Maandamano ya Spika, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katibu wa Bunge, yaliingia Ukumbini)

KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa shughuli zilizopangwa kwa ajili ya Mkutano wa Ishirini wa Bunge la Tisa zimekamilika.

SPIKA: Ahsante sana Katibu wa Bunge, kama nilivyowataarifu hapo awali leo tarehe 16 Julai, 2010, saa za Alasiri Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, atakuja kulihutubia Bunge na sasa amekwishafika, Mheshimiwa Rais karibu kwa hotuba yako. *(Makofi)*

HOTUBA YA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MHE. JAKAYA M. KIKWETE, AKIHUTUBIA BUNGE LA TISA, 2005 - 2010

RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia uzima na kutuwezesha kushuhudia siku hii ya kihistoria ambapo Bunge la Tisa linamaliza kipindi chake cha miaka mitano. Nimekuja hapa kutimiza wajibu wa kikatiba wa kuhitimisha shughuli za Bunge hili, ili kufungua milango kwa mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa kuwapata Wabunge wengine na Rais wa kipindi kijacho kuanza rasmi.

Mheshimiwa Spika, katika kuagana na Wabunge, Bunge lako Tukufu, ambalo nami ni sehemu yake, ninayo mengi ya kukushukuru na ninao wengi wa kuwakushukuru. Kwanza ni Watanzania wenzangu wote. *(Makofi)*

Watanzania walionipa fursa hii adhimu ya kuwatumikia katika nafasi hii ya juu kabisa ya uongozi wa nchi hii. Nawashukuru kwa ushirikiano wao mkubwa kwangu na Serikali yangu na kwa Bunge letu Tukufu katika kipindi chote cha miaka mitano.

Nawashukuru pia kwa kutimiza wajibu wao wa kiraia wa kushiriki kwa ukamilifu katika shughuli mbalimbali za maendeleo za kuijenga nchi yetu. Natambua na kuthamini uvumilivu na uelewa wao wakati nchi yetu ilipokuwa inapita katika vipindi vigumu. Nawashukuru sana hata wakati huo Watanzania wenzangu wameunga mkono wameiunga mkono Serikali yetu na kutusaidia sana, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru viongozi wenzangu wakuu na watendaji wakuu wa Serikali na Mashirika yake. Napenda kuwatambua kwa ajili hiyo Makamu wa Rais Dr. Mohamed Ali Shein, ambaye pia ningependa kuchukua nafasi hii kumpongeza kwa kuteuliwa kuwa mgombea wa Urais wa Zanzibar, tunamtakia kila la heri ili apate ushindi mnono, aweze kuongoza Zanzibar na kuwa sehemu ya uongozi wa Jamhuri ya Muungano.

Napenda kumshukuru Mheshimiwa Aman Abeid Karume, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Nampongeza sana kwa kutimiza salama kipindi chake cha uongozi, namtakia kila la heri katika shughuli zake atakazozifanya wakati atakapokuwa amestaafu. (*Makofi)*

Pia, namshukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda. Namshukuru sana yeye kwa kiasi alichonisaidia lakini namshukuru sana kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kuwa kiongozi wa shughuli za Serikali hapa Bungeni. Namshukuru pia Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyemtangulia Mheshimiwa Edward Lowassa, ndiye tuliyeanza naye amepata ajali njiani, lakini kuvunjika kwa koleo siyo mwisho uhunzi. *(Makofi)*

Namshukuru Waziri Kiongozi, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha. Aidha, nawashukuru Mawaziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu Kiongozi, Ndugu Phillemon Luhanjo, Katibu Wakuu, Naibu Katibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na watendaji waandamizi katika Serikali na katika Halmashauri za Wilaya. Msaada wao, ushirikiano wao na uchapakazi wao ndiyo uliotuwezesha kupata mafanikio tunayojivunia leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, natoa shukrani maalum kwako kwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu. Nakushukuru wewe kwa uongozi wako mahiri wa Bunge letu hili. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri walioifanya ya kuwawakilisha wananchi waliowatuma, nawashukuru kwa ushirikiano wenu na msaada wenu kwangu na kwa Serikali yetu. *(Makofi)*

Bunge letu limekuwa ni kielelezo cha ustawi wa demokrasia yetu nchini, mmetoa hoja nyingi nzuri za kukosoa na kuishauri Serikali. Kuna baadhi ya nyakati maneno yalikuwa makali, wakati mwingine yalikuwa yanaelekea kuvuka mipaka ya staha, lakini nasema kwamba sina mfundo na yeyote. Kwa maana sina kinyongo na yeyote, mimi naamini kuwa ilikuwa ni kwa nia njema, isitoshe elimu haina mwisho na wakati mwingine kuteleza ndiyo kujifunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shukrani zangu za mwisho lakini sio mwisho kwa umuhimu ziwaendee wakuu wa vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama, kwa Majeshi, General

Davis Mwamnyange, Mkuu wa Jeshi la Polisi na Wanajeshi na Askari wote na watumishi wote wa ulinzi wa Jeshi la Ulinzi na Usalama. Tunamaliza kipindi chetu nchi ikiwa salama, mipaka iko salama na usalama wa maisha na mali za raia ni za uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipokuja kuzindua Bunge hili tarehe 30 Desamba, 2005 nilielezea na kufafanua kwa kina dira, mwelekeo na malengo ya Serikali ya Awamu ya Nne. *(Makofi)*

Niliahidi kwamba Serikali ninayoingoza ingeongozwa na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kama dira yetu. Ilani imetoa majukumu mahususi kwa Serikali kufanya kupitia kwenu Waheshimiwa Wabunge mliwaahidi Watanzania mambo kumi yafuatayo katika miaka mitano yetu ya Serikali:-

(i) Serikali itahakikisha kuwa amani, utulivu na umoja wa nchi yetu na watu wake vinadumishwa;

(ii) Tutadumisha na kuendeleza mafanikio yaliyopatikana tangu Serikali ya Awamu ya Kwanza hadi leo;

(iii) Tutaendeleza vita dhidi ya umaskini, ujinga na maradhi, kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya;

(iv) Tutatimiza ipasavyo wajibu wetu wa utawala na maendeleo na tutaendesha dola kwa misingi ya utawala bora na uwajibikaji, utawala wa sheria unaoheshimu na kulinga haki za binadamu;

(v) Serikali itaimarisha uwezo wake wa kulinda maisha na mali za raia na tutapambana na uhalifu wa kila aina na majambazi hatutayaacha yatambe yatakavyo;

(vi) Tutahakikisha mipaka ya nchi yetu ipo salama, hatutamruhusu mtu yeyote au nchi yoyote kuchezea mipaka ya nchi yetu na uhuru wetu; *(Makofi)*

(vii) Nilisema tutafanya kila tuwezalo kuhakikisha kuwa Tanzania ina mahusiano mazuri na mataifa yote dunia na mashirika yote ya kimataifa na ya kikanda;

(viii) Serikali itajali sana maslahi na mahitaji ya makundi maalum katika jamii hususan wanawake, vijana, watoto, wazee, walemavu na yatima;

(ix) Itaongoza mapambano mapya ya kuhifadhi mazingira ili vizazi vijavyo virithi nchi iliyokuwa nzuri na misingi imara ya maendeleo yaliyo endelevu; na

(x) Tutaendeleza michezo na shughuli za utamaduni na burudani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo naona fahari kusema kuwa tumepiga hatua kubwa katika kutekeleza malengo yetu hayo na mambo mengine mbalimbal tuliyoahidi katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala au yaliyojitokeza kwa nyakati au mahali mbalimbali. Unakwenda mahali unawambiwa daraja basi unaahidi, halafu unahangaika nalo. Viwango vya mafanikio vinatofautiana kwa kila sekta hata hivyo tumesonga mbele kwa kasi ya kuridhisha japo bado tuna safari ndefu ya kuelekea kwenye maisha bora kwa kila Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapoangalia mafanikio makubwa tuliyoyapata katika kipindi hiki na kulinganisha na changamoto tulizokabiliana nazo katika kipindi hiki, kwa kweli huwa nastaajabu na kujiuliza tumewezaje? *(Makofi)*

Mimi sio Sheikh na wala sio mwanazuoni katika dini yangu, ni mcha Mungu wa kawaida maamuma. Lakini naamini ni rehema za Mwenyezi Mungu tu ndizo zilizotuwezesha kupata mafanikio tunayojivunia leo hii hapa nchini. Lazima kuna mkono wake. Kama mnavyojua tulianza kazi nchi ikiwa katikati ya ukame mkubwa, ukame wa aina yake kutokea tangu tupate uhuru. Kukawa na upungufu mkubwa wa chakula takribani watu wapatao 3,776,000 walipatiwa chakula na Serikali. Ukame huo pia ulikausha maji katika mabwawa yetu ya kuzalisha umeme, hivyo tukawa na upungufu mkubwa wa umeme na tukalazimika kukodi vinu vya kufua umeme kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, kuanzia katikati ya mwaka 2007, bei za mafuta zilipanda kwa kasi sana na ilipofikia Juni, 2008, zilifikia kiwango cha juu ambacho hakijawahi kufikiwa duniani, pipa moja dola 147. Mafuta kama mnavyojua yanagusa nyanja zote za maisha ya binadamu, hivyo gharama za usafiri na uchukuzi zilipanda, gharama za uzalishaji mashambani zilipanda, bei ya *diesel* ilipanda. Kwa hiyo, kulima katika hekari moja kwa trekta ilipanda.

Pia, gharama za shughuli za viwanda nazo zikapanda, utoaji wa huduma mbalimbali pia ukapanda kwa ajili hiyo. Hali hiyo, ilisababisha mfumko wa bei na gharama za maisha kupanda sana hapa nchini.

Katika nusu ya pili ya mwaka 2008, dunia ikakumbwa na tatizo jingine kubwa la machafuko katika masoko ya fedha ya Kimataifa, yaliyosababisha kudorora kwa uchumi wa dunia, *World Economic Recession*.

Kudorora huko kulisababisha bidhaa zetu tunazouza nje kukosa masoko, na zile kidogo tunazouza bei yake imeporomoka sana na kuwatia hasara wazalishaji na wafanyabiashara wetu. Watalii kutoka nje wakapungua, wawekezaji walikuwa wameonesha nia ya kuja kuwekeza nchini lakini wakaahirisha kufanya hivyo. Kwa ujumla utulivu wa uchumi wetu ulianza kuyumba, ukuaji wa uchumi ukashuka kuliko

matarajio, mfumko wa bei ukapanda sana, mapato ya Serikali yakawa chini ya lengo na kadhalika.

Ili kulinusuru taifa ninyi mnakumbuka, Serikali ililazimika kutengeneza mpango wa dharura wa kuunusuru uchumi ambao tulitumia shilingi bilioni 1, trilioni 1.7 ambazo hazikuwa kwenye mpango. Hatua hiyo ndiyo iliyosaidia kupunguza makali ya athari za kudorora kwa uchumi hapa nchini. Wahenga wanasema kila msiba una mwenziwe.

Katika baadhi ya mikoa hasa ile inayopakana na Kenya mwaka 2008/2009 ulikuwa ni wa ukame mkali uliosababisha hata mifugo na wanyamapori kufa, watu wake wakawa maskini na kukabiliwa na njaa kali lakini Serikali ikabeba mzigo wa kuwalisha Ndugu zetu wa Longido, Monduli na kwingineko. Sasa tunaangalia namna ya kuwasaidia waanze maisha mapya kwani Mmasai Ng'ombe, Mmasai asipokuwa na Ng'ombe si Mmasai tena atabaki na lubega tu, lakini lubega ni kwa ajili ya kuchunga Ng'ombe. Kwa hiyo, tutajaribu kuona ni namna gani tunaweza kuwasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya mvua kubwa zilizonyesha mkoani Dodoma, Desemba 2009 nakumbuka ilikuwa tarehe 23 katikati ya Kilosa na Mpwapwa, sehemu kubwa ya Reli ya Kati ilisombwa na maji, imetuchukua takribani miezi sita mpaka Treni zilipoanza tena kazi. Matatizo yote hayo niliyoyataja yamekuwa na athari kubwa kwa ukuaji na ustawi wa uchumi wa nchi yetu, yameturudisha nyuma kwa kiasi kikubwa kwani kama athari hizo zisingekuwepo tungekuwa tumefikia malengo yetu mengi na hata kuyavuka.

Hata hivyo, tumepata mafanikio ya kutia moyo kwenye nyanja mbalimbali jambo linalotuthibitishia kuwa sera zetu za uchumi ni sahihi. Uchumi wetu umeweza kujenga kiwango cha uhimilivu yaani *perseverance* hata tumeweza kuhimili misukosuko ya uchumi kama iliyotukumba hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania imeendelea kuwa nchi tulivu, yenye amani, usalama na watu wake wana umoja licha ya tofauti zao za kidini, kikabila, rangi na ufuasi wa vyama vya siasa. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita tumejitahidi kadri ya uwezo wetu kulinda, kuendeleza na kuimarisha sifa hii njema ya nchi yetu. Nawashukuru sana Watanzania wenzangu kwa kutambua haraka na kuepukana na vihatarishi vya amani na umoja wa nchi yetu. Nawashukuru na kuwapongeza kwa kuwapuuza wale wote wanaohangaika usiku na mchana, maana kuna watu usiku na mchana wanahangaika kuwagawa Watanzania kwa dini zao, kwa makabila yao, Ubara na Uzanzibari, Upemba na Uunguja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, umoja wa nchi yetu una sura mbili, kwanza ni umoja baina ya Watanzania kwa makabila, rangi, dini na vyama mbalimbali. Pili ni Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar uliozaa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Muungano wetu umeendelea kuwa imara na katika kipindi cha miaka mitano hii tumechukua hatua mahsusi za kuimarisha Muungano na mshikamano wetu. Tumeimarisha Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kumteua Waziri maalum katika Ofisi hiyo atakayekushughulikia masuala ya Muungano, tumeboresha taratibu za majadiliano ya masuala ya Muungano kwa

kumfanya Makamu wa Rais kuwa Mwenyekiti wa vikao vya pamoja kati ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi. Mnajua tunayo Kamati ya pamoja, Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi walikuwa wanakutana, tulichokifanya katika safari hii ni kuhakikisha kwamba sasa wanapokutana basi Makamu wa Rais awe ndiye Mwenyekiti wao kuwakutanisha pande hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, vikao vitano vilifanyika na mambo mengi yalizungumzwa na kupatiwa ufumbuzi. Aidha, vikao 75 vya ushirikiano wa sekta zisizo za Muungano pia vilifanyika maana kuna zile sekta ambazo ni za Muungano halafu kuna mambo ambayo si ya Muungano, lakini kila linalotokea huku linahusu upande mwingine, hawa nao pia walifanya vikao vyao vipatavyo 75. Tumefanikiwa na mambo mengi yamezungumzwa lakini yaliyobakia ni kidogo sana ambayo pia tutayamaliza katika kipindi kitakachofuata.

Siku ile ya tarehe 30 Desemba, 2005 nilielezea kwa kusononeshwa kwangu na mpasuko wa kisiasa uliopo Zanzibar. Niliahidi kufanya kila niwezalo ili hali hiyo ibadilike na Wazanzibar wawe wamoja, waishi kwa upendo, amani na utulivu. Bila shaka mtakubaliana nami kwamba tumefika mahali pazuri na ishara njema zinaonekana. Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza Viongozi wenzangu wa Chama cha Mapinduzi na wenzetu wa Chama cha Wananchi *CUF* kwa kukubali vyama vyetu viwili vizungumze kwa sababu matatizo ni yetu sisi, sisi wenye matatizo wenyewe sisi ndiyo jawabu yaani *We are source of the problem, we are also part of the solution.*

Nawaashukuru na kuwapongeza kwa dhati Mheshimiwa Dr. Aman Abeid Karume, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, nampongeza sana Mheshimiwa Seif Sharif Hamad maarufu kwa jina la Maalim Seif, Katibu Mkuu wa *CUF* kwa maridhiano ya tarehe 5 Novemba, 2009. Maridhiano hayo yamefungua njia ya kuwezesha kutekelezwa makubaliano ya vyama vyetu. Nawapongeza kwa dhati Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kukubali kura ya maoni ifanyike ili wananchi wa Zanzibar waamue kuhusu kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa baada ya uchaguzi ili watoke kwenye mazingira hayo yaliyokuwepo. *(M akofi)*

Naendelea kuahidi ushirikiano wangu na msaada wangu pale unapohitajika, nawasihi ndugu zangu wa Zanzibar tuitumie fursa hii ya kihistoria kuzika siasa za uhasama, kuzima mazingira ya kushupaliana yaliyowagawa wananchi wa Zanzibar katika makundi ya uadui na badala yake Wazanzibar wawe wamoja wanaoishi kindugu na kushirikiana. (*Makofi*)

Narudia kutoa pongezi zangu kwa Rais Karume kwa kumaliza salama na mafanikio makubwa ya kipindi chake cha miaka kumi ya uongozi Zanzibar, Wazanzibar watamkumbuka Rais Abeid Aman Karume, kwa mema mengi aliyoifanyia Zanzibar. Tumtakie afya njema na umri mrefu wakati huohuo nampongeza tena yaani ninarudia kumpongeza Dr. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa mgombea wa Urais Zanzibar kwa tiketi ya CCM. (*Makofi*)

Mheshimiwa Ali Mohamed Shein ni kiongozi mtulivu asiyekuwa na papara, ni kiongozi makini, mwadilifu na mpenda maendeleo. Naamini akichaguliwa kuwa Rais wa

Zanzibar, maana naamini itakuwa hivyo, atadumisha na kuendeleza yale yote mema yaliyofanywa katika vipindi vilivyopita kutoka awamu ya kwanza mpaka awamu ya sita na kuisogeza Zanzibar katika hatua nyingine mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imeendelea kuwa kielelezo kizuri cha utulivu wa Siasa na ukomavu wa Demokrasia Barani Afrika. Katika miaka mitano iliyopita tumefanikiwa kuhakikisha kwamba uhuru wa kisiasa, uhuru wa kutoa maoni, uhuru wa vyombo vya habari na uhuru wa kuabudu umeheshimiwa na kulindwa. Tumehakikisha kwamba wanasiasa pamoja na vyama vya siasa, asasi zisizokuwa za Kiserikali ama asasi za wananchi *Civil Society* na wananchi wote kwa ujumla wanafaidi haki zao za msingi.

Tumefanya jitihada kuhakikisha kwamba uwanja wa ushindani wa kisiasa unawekwa sawia kwa ajili hiyo tumefanya marekebisho ya Sheria zetu za Uchaguzi, tumetoa ruzuku kwa vyama vya siasa vyenye Madiwani kuanzia mwaka 2007.

Sasa hivi chama kisichopata ruzuku yoyote ni kile ambacho kimeshindwa hata kupata Diwani mmoja, hali hii imedhihirisha ukomavu wa kisiasa nchini na tumwombe Mwenyezi Mungu tuendelee katika hali hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahadi yangu ya kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya rushwa, ubadhirifu wa mali ya umma na matumizi mabaya ya madaraka nchini tumeitimiza. Tumekemea vitendo vya kutoa na kupokea rushwa na kuchukua hatua za kisheria na kinidhamu kwa wahusika pale ilipobidi kufanya hivyo.

Tumetunga Sheria mpya na kali zaidi na tumepitisha mkakati mpya wa kupambana na rushwa, tumeunda upya chombo cha kuzuia na kupambana na rushwa na sasa TAKUKURU ina Ofisi katika kila Wilaya na tumeiongezea uwezo wa kibajeti na kirasilimaliwatu na vitendea kazi. Juhudi hizo zinadhihirisha utashi wa kisiasa tulionao wa kupambana na rushwa na matumizi mabaya ya madaraka. Kwa sababu hiyo, katika miaka mitano hii tuhuma nyingi zimechunguzwa, kesi nyingi zimefikishwa Mahakamani ikiwa ni pamoja na zile kesi za rushwa kubwa na mapambano bado yanaendelea. (*Makofi*)

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita tumepeleka Mahakamani kesi 780 na katika kipindi cha miaka mitano hii Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali imeimarishwa kiutendaji na kisheria.

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2008 Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria mpya inayotoa uwezo na uhuru mkubwa zaidi kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali na Ofisi yake.

Nilianzisha utaratibu wa Watendaji Wakuu wa Wizara, Halmashauri za Wilaya na Miji, Idara za Serikali na Wakala mbalimbali kusoma na kujadili taarifa za mwaka za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu maeneo yao maana taarifa hizi zilikuwa zinatolewa lakini zilikuwa hazizungumzwi. Unasema imetoka ile taarifa, ndiyo!

unasema basi, kwani ina nini? Anasema Mzee ni kawaida tu yaleyale, wewe humjui Mkaguzi?

Nimesema safari hii zizungumzwe tuunde Kamati za Kiwizara, za Halmashauri, za Watendaji na Viongozi Wakuu kukaa na kuzungumza zile taarifa wayabaini matatizo na kasoro zilizotajwa mle ndani na wachukue hatua. Utaratibu huu unazifanya taarifa hizi kuwa na thamani lakini pia umesaidia kuboresha Hesabu za Serikali katika maeneo mbalimbali. Siku hizi wanaopata Hati Chafu wamepungua sana, nampongeza sana Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Ofisi yake kwa kazi nzuri wanayoifanya, utaratibu huu pia umetusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nampongeza sana Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa uamuzi wa sasa kuanza kufanya ukaguzi wa thamani ya fedha yaani *Value for Money Audit* ili kulinganisha fedha iliyotumika na kazi iliyofanyika. Hii ni hatua muhimu itakayosaidia kuhakikisha kuwa fedha za Umma zinatumika vizuri na kwa shughuli iliyokusudiwa kwa sababu unapokagua vitabu unaangalia vilivyoandikwa. Kwa hiyo, kama *voucher* unaziona, *entry* zimekuwa nzuri, nasema Hati Safi. Lakini pengine kilichoandikwa kwenye kile kitabu cha hesabu sicho kilichopo *on the ground*, umeambiwa daraja limejengwa lakini daraja halipo hela zimekwishaliwa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, sasa ukaguzi huu wa *value for money audit* ndiyo utatufikisha katika kuwianisha hesabu zilizopo kwenye vitabu na kazi iliyofanyika. Naamini Wabunge wale wa Kamati ya Mheshimiwa Dr. Willibrod P. Slaa wameona, vitabu vimeandikwa vizuri lakini daraja, shule, Zahanati na barabara pia hazipo, ndiyo maana hii ni muhimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki pia tumeanza utaratibu mzuri wa kuwawajibisha wale wote wanaohusika na wizi na ubadhirifu wa fedha za Umma mara unapogundulika na Wakaguzi. Tofauti na zamani ambapo hatua husubiri baada ya taarifa ya ukaguzi kuwasilishwa Bungeni, maana inakuja hapa inajadiliwa na wakati mwingine inaletwa mwishoni mwa kikao watu wana haraka ya kuondoka. Jamani imepokelewa haya waliohusika waendelee kurekebisha kasoro! Au Mbunge mmoja ana Waziri mmoja ambaye ana *soo* naye basi anamkomalia huyo huyo. Kwa hiyo sasa, tumesema hivi wakikagua wakiona kwamba hapa hesabu inaonyesha kwamba kuna wizi nimewaambia watoe ripoti Polisi, TAKUKURU nao nimeshawaagiza wachukue hatua za kisheria badala ya kungoja wakakae kwenye Halmashauri. Halmashauri inakutana wanasema kwani hakuna kusameheana? Basi aliyeiba anaachiwa.

Mheshimiwa Spika, tumejitahidi kusimamia vema Sheria ya Manunuzi kwa nia ya kupunguza mianya ya rushwa katika manunuzi ya Serikali hasa kwenye mikataba. Tumefanya mapitio ya Sheria hiyo na kuainisha maeneo yanayohitaji kufanyiwa marekebisho ili kuimarisha. Bahati mbaya katika uhai wa Bunge hili Muswada huo haukuweza kuwasilishwa Bungeni lakini ni matumani yetu kuwa mapema katika Bunge lijalo yatawasilishwa na uamuzi kufanyika ili tuimarishe Sheria yetu ya manunuzi.

Mheshimiwa Spika, niliahidi kulipa msukumo mpya suala la maadili ya uongozi, tumeruhusu mijadala ya wazi miongoni mwa wananchi, vyama vya hiari, vyombo vya habari na hata hapa Bungeni kuhusu maadili ya uongozi wa Umma. Tumeimarisha Tume ya Maadili ya Viongozi na kuijengea uwezo zaidi wa kisheria na kifedha, Tume ya Maadini ya Viongozi ina Mamlaka siyo tu ya kupokea fomu za mali walizojaza Viongozi bali pia ina uwezo wa kuhakiki mali hizo ili kuthibitisha uwezo wa taarifa zinazotolewa. Tumebadili pia utaratibu na kuamua kwamba hata mali za familia nazo zikaguliwe ili kuthibitisha ukweli, hii ni kujaribu kuwabana tu wale Viongozi wasiokuwa waadilifu wapate taabu ya kuficha mali zao walizozipata kwa njia zisizokuwa za halali. Naamini tukiendelea na mwenendo huu, maadili ya Viongozi wetu yatakuwa yamejengeka katika msingi mzuri.

Mheshimiwa Spika, niliahidi kwamba tutatafuta utaratibu wa kudhibiti mapato na matumizi ya fedha katika Uchaguzi ili uongozi usiwe bidhaa ya kununuliwa au kura ya mtu isiwe bidhaa ya kuuza. Tayari tunayo Sheria ya gharama za Uchaguzi imepitishwa na itaanza kutumika katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu. Mimi ninaamini kwamba, pamoja na upya wake itasaidia kupunguza au hata kukomesha vitendo vya rushwa katika Uchaguzi na mbele ya safari kama kuna upungufu tutaiimarisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, tumefanikiwa kuimarisha utawala bora. Katika utendaji kazi, tumeendesha shughuli za Serikali kwa kuheshimu mgawano wa madaraka baina ya mihimili mikuu ya dola, Bunge; Mahakama na Utawala. Sisi katika Serikali tumeendelea na wajibu wetu wa uwezeshaji wa mihimili hiyo.

Mheshimiwa Spika, kama mtakavyokumbuka, Mfuko wa Bunge tayari umeanzishwa na umelipa Bunge uhuru zaidi kwa bajeti yake. Tumeendelea kuongeza bajeti ya Bunge na sasa ni mara mbili ya ile tuliyoikuta mwaka 2005. Maslahi ya Waheshimiwa Wabunge nayo tumeyaboresha, Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, nao umeanzishwa ili kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge waweze kushughulikia matatizo madogo madogo yanayowakabili wananchi wao. Mazingira bora tuliyoyajenga, yameliwezesha Bunge letu katika miaka mitano hii kufanya kazi kwa uhuru zaidi, uwazi zaidi na kwa mafanikio zaidi. Bunge letu ni kielelezo cha ukomavu na ustawi wa demokrasia yetu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeimarisha Mahakama na vyombo vya utoaji wa haki. Ni ukweli ulio wazi kuwa amani na utulivu hustawi kama haki itatendeka na itaonekana inatendeka kama wanavyosema wenyewe Wanasheria. Tumetimiza ahadi yetu na wajibu wetu wa kuiwezesha Mahakama kufanya shughuli zake kwa ufanisi zaidi. Mahakama imeendelea kuwa huru na kamwe Serikali haijaingilia Mahakama katika shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, tumeongeza idadi ya Majaji, Mahakimu na Mawakili wa Serikali na ninafurahi tumezingatia uwakilishi wa kijinsia katika Mahakama. Katika kipindi change, nimetua Majaji 12 wa Mahakama ya Rufaa, kati yao wanne ni Wanawake, Majaji 51 wa Mahakama Kuu, Wanawake 24, tumeajiri Mahakimu Wakazi 256 kati ya hao Wanawake ni 117, tumeajiri Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo 394

kati ya hao 134 ni Wanawake. Majaji na Mahakimu Wanawake wamekuwa wengi kuliko wakati mwingine wote katika historia ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumetekeleza ahadi ya Ilani ya Uchaguzi ya kuongeza idadi ya Wanawake katika nafasi za maamuzi. Kwa ujumla, hapa nchini sasa tumefikia asilimia 31 kutoka asilimia 26 mwaka 2005. Hivi leo tuna wanawake wengi kwa nafasi za Ubunge, Uwaziri, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi Watendaji na kadhalika. Ninafurahi na kushukuru kwamba, wanawake hawa wengi hawajaniangusha, wanafanya kazi zao vizuri na ni wachapa kazi hodari na pia ni waaminifu. *(Makofi/Vigelele)*

Mheshimiwa Spika, tutaendelea na kazi ya kuboresha bajeti ya Mahakama ingawaje kiasi kilichotengwa mpaka sasa ni kidogo ukilinganisha na mahitaji lakini tunaahidi tutaendelea kufanya vizuri zaidi. Tumeboresha maslahi ya Majaji na Mahakimu na tunakusudia kufanya vizuri siku za usoni. Hivi sasa tunaendelea na mchakato wa kuiwezesha Mahakama nayo kuwa na Mfuko wake maalum kama inavyotaka Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ufanisi na utendaji wa Serikali unategemea kuwepo rasilimali watu wenye ari ya kuchapa kazi na wenye vitendea kazi stahiki. Katika hotuba yangu ya kufungua Bunge, nilielezea pia kwamba, tutachukua hatua za kuboresha maslahi ya Watumishi wengine. Niliunda Tume Maalum ambayo ilitupatia mapendekezo mengi mazuri. Tumekuwa tunayafanyia kazi na kuyatekeleza kadiri uwezo wa kibajeti ulivyotokea.

Mheshimiwa Spika, katika miaka mitano (5) iliyopita, tumewapandisha vyeo watumishi 140,797 ambao katika miaka mingi huko nyuma walikuwa hawajapandishwa vyeo walivyostahili kupata. Kwa sababu ya kufanya hivyo, ilibidi pia turekebishe na stahili zao. Katika kipindi hiki tumetumia shilingi bilioni 108 kwa ajili ya kuwalipa haki zao wafanyakazi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitumia shilingi bilioni 45 kulipia malimbikizo ya madeni halali ya Walimu. Bado kuna rufaa za madai kama shilingi bilioni sita ambazo zinaendelea kushughulikiwa. Katika kipindi hiki pia tumepandisha kima cha chini cha mshahara kutoka shilingi 65,000 mpaka shilingi 135, 000 sawa na ongezeko la asilimia 107. Bado kiwango hicho ni kidogo ukilinganisha na mahitaji halisi. Ahadi yetu ni kwamba, tutaendelea kuongeza kiwango hicho kwa kadri uwezo wa kibajeti utakavyojitokeza.

Mheshimiwa Spika, tumeboresha mafao ya uzeeni kwa watumishi kwa kuboresha taratibu za ukokotoaji wa mafao za *LAPF, PSPF* na *PPF*. Tumeboresha utendaji katika Halmashauri zetu kimuundo, kifedha na kiutumishi ili ziweze kuwa kichocheo cha kasi ya maendeleo ya haraka ya watu wetu. Katika kipindi cha miaka mitanoiliyopita, tumeongeza ruzuku katika Halmashauri za Wilaya kwa karibu mara tatu, kutoka shilingi bilioni 780 mwaka 2005 hadi shilingi bilioni 2,728 kwa mwaka. Ilikuwa ni shilingi

bilioni 780 sasa Halmashauri ni shilingi trilioni mbili na milioni 728. Tumeajiri Wahasibu 795 na Wakaguzi wa Ndani 447 ili kuboresha huduma za kiuhasibu katika Halmashauri. Wahandisi 95 wa maji wameajiriwa, Watumishi wa kada mbalimbali za afya 6,437 wameajiriwa, watumishi hawa na ruzuku tunayotoa wamechangia kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Kazi ya kuboresha utendaji wa Halmashauri bado ipo kubwa mbele yetu hasa ile ya kuzuia wizi na ubadhirifu. Tumeanza Awamu ya Pili ya Maboresho ya Serikali za Mitaa na ni matumaini yangu kuwa suala hilo litapewa uzito unaostahili.

Mheshimiwa Spika, ulinzi na usalama wa nchi yetu uliendelea kuwa ajenda yetu kuu katika miaka mitano hii. Nilipokuja kulifungua Bunge, niliahidi kwamba, Serikali ya Awamu ya Nne itajenga mazingira mazuri ya kazi kwa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. Kazi hiyo tumeifanya na tunaendelea nayo. Tumeviwezesha vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kifedha na kivifaa ili viweze kumudu majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, tumeendelea kuboresha makazi ya Wanajeshi wetu, tumeendelea pia kuboresha maslahi ya Wanajeshi wetu, lakini bado changamoto kubwa tuliyokuwa nayo kwa Wanajeshi wetu hawa ni kuzidi kuimarisha Jeshi letu kwa zana na vifaa na kazi hiyo tunaendelea nayo. Hata hivyo, hapa tulipofikia, ni mahali pazuri na ndiyo maana niliwapongeza Wanajeshi wetu. Niliahidi kwamba tutaanza kushiriki katika shughuli za ulinzi wa amani duniani iwapo tutaombwa kufanya hivyo. Nafurahi kusema kwamba, tumepeleka walinzi wa amani Lebanon na Darfur. Vilevile mwaka 2008, Jeshi letu kwa kuagizwa na Umoja wa Afrika *(AU)* limefanya kazi nzuri ya kurejesha umoja katika Visiwa vya Comoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uhalifu wa kutumia silaha bado ni changamoto kwa usalama wa watu na mali zao. Tulipoingia madarakani, tulikuta wimbi kubwa sana la uhalifu, tuliahidi kwamba hatutaacha majambazi watambe. Kazi hiyo tumeifanya, Jeshi la Polisi limefanya kazi kubwa na nzuri. Uhalifu bado upo lakini siyo kama ilivyokuwa zamani na sifa moja ni kwamba, siku hizi tukio likitokea haipiti kipindi kirefu wahusika wanatiwa nguvuni na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005, niliahidi kwamba, tutaongeza kasi ya kuwarudisha makwao Wakimbizi waliopo nchini, ahadi hiyo tumeitimiza. Wakimbizi 483,804 wamerudi kwao na kambi 12 za Wakimbizi zimefungwa, lakini kuna Wakimbizi 1,423 kutoka Somalia, na Wakimbizi 160,000 kutoka Burundi walioomba kubakia nchini. Wengi wa hawa hawana pa kwenda kwa sababu hawakujui pa kwenda. Wametoka huko mwaka 1965, wengine mwaka 1972, wamezaliwa hapa, hawajui pa kwenda. Serikali yetu ikafanya wajibu wake wa kihistoria wa kuwakubali wapewe uraia kwa masharti ya Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya uchumi, tuliwaahidi Watanzania kwamba katika miaka mitano ya uongozi wetu, tutaendeleza jitihada za kukuza na kujenga uchumi wa kisasa ulio endelevu ili kupunguza umaskini na kuboresha hali ya maisha ya Watanzania. Katika miaka mitano iliyopita, tumeendelea kusimamia vizuri Sera za

Uchumi Jumla *(Micro-economic Policies)* pia tumetunga na kuboresha Sera za Jisekta na Sheria mbalimbali ili kurahisisha ushiriki wa sekta binafsi na wananchi kwa ujumla katika shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, pato la Taifa limeongezeka kutoka shilingi trilioni 15.9 mwaka 2005 hadi kufikia shilingi trilioni 28.2 mwaka 2009 kwa bei za miaka husika. Kwa ajili hiyo, pato la wastani la Watanzania limeongezeka kutoka shilingi 441,030 mwaka 2005 hadi shilingi 693,185 mwaka wa jana. Kasi ya wastani ya ukuaji wa pato la Taifa imekuwa kwa 6.9% katika kipindi hicho. Kasi hiyo ingekuwa kubwa zaidi kama uchumi wetu usingekabiliwa na matatizo ya ukame, upungufu mkubwa wa umeme, kupanda sana kwa bei za mafuta, kudorora kwa uchumi wa Taifa na kuharibika kwa reli yetu. Pamoja na hayo, hatuna budi kujipongeza kwani, uchumi wetu kukua kwa 6% mwaka 2009 na wastani wa 6.9% katika kipindi hiki, ni mafanikio makubwa kwa viwango vyote unavyoweza kuvitumia duniani. Hapa duniani, uchumi wowote unaokua kwa 6% ni miongoni mwa uchumi unaohesabiwa kwamba unakua kwa kasi kubwa sana. Kwa hiyo na sisi tuko kwenye kundi hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeshaeleza, ni usahihi wa Sera zetu za Uchumi na uhimilivu wa Serikali. Uchumi umeendelea kuwa tulivu, hivi viashiria vyote vilikuwa imara isipokuwa mfumko wa bei. Mapato yetu ya fedha za kigeni yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 2994.9 mwaka 2005 hadi kufikia shilingi bilioni 4693.6 mwaka wa jana. Akiba yetu ya fedha za kigeni kwa ajili hiyo imeongeza kutoka shilingi bilioni 2.21 mwaka 2005 na mwaka wa jana tukafikia shilingi bilioni 3.55 ambazo inatuwezesha kuagiza bidhaa kwa miezi sita.

Mheshimiwa Spika, katika miaka mitano hii, udhibiti wa mfumuko wa bei, ulikuwa ni changamoto yetu kuu hasa kuanzia mwaka 2007 baada ya bei za mafuta kupanda sana. Mfumuko wa bei ulipanda kutoka asilimia tano mwaka 2005 na kufika wastani wa asilimia 12.1 mwaka 2009. Kutokana na juhudi tulizozifanya kudhibiti ujazi wa fedha na hali nzuri ya chakula mwaka huu, mfumuko wa bei umeanza kuonesha dalili ya kushuka. Hadi Juni ilikuwa ni asilimia 7.2 na hali ya upatikanaji wa chakula ikiendelea kuwa nzuri na kama machafuko hayatatokea tena kwenye bei za mafuta, tutafanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, miaka mitano hii, tumeongeza mapato ya ndani kwa zaidi ya mara mbili. Wastani wa mapato ulikuwa ni shilingi bilioni 177.1 mwaka 2006/2006, mwaka huu tumefikia shilingi bilioni 390 kwa mwezi. Hii imetupa uwezo wa kuongeza bajeti ya Serikali kutoka shilingi trilioni 4.13 mwaka 2005/2006 na kufikia shilingi trilioni 11.6 mwaka wa fedha 2010/2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, tumeendelea kupunguza utegemezi kwa wafadhili katika bajeti ya Serikali kutoka asilimia 44 mwaka 2005, mwaka huu tuko asilimia 28. Hivyo safari ya kupunguza utegemezi tumekuwa tunaifanya kwa mafanikio kama tulivyoahidi. Kwa sababu makusanyo ya mapato ni upande mmoja, lakini nidhamu katika matumizi ni jambo lingine. Kama nilivyoahidi, tumefanya jitihada kubwa katika

usimamizi wa ufanisi wa matumizi ya fedha za Serikali. Nimeeleza awali hatua tulizochukua kuimarisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* na pia nimeeleza uamuzi tuliofanya kwamba hesabu hizo zisomwe na makosa yaliyobainika yachukuliwe hatua. Pia tumechukua hatua za kubana mianya ya ubadhirifu na utekelezaji mbovu wa miradi ya Serikali. Nimeshaeleza wizi na ubadhirifu unapogundulika, tumeagiza TAKUKURU na Polisi wachukue hatua kwa wahusika bila ya ajizi. Hatua zimekwishachukuliwa na kesi zipo zinazoendelea Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, tulipokutana mara ya kwanza, niliainisha majukumu manane ya Serikali katika kutengeneza mazingira mazuri katika uchumi kukua na biashara kustawi. Tumeandaa Sera mbalimbali na kurekebisha baadhi ya Sheria ili kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kuwezesha uchumi kukua na tumetengeneza mfumo bora wa fedha. Pia tumeweka mifumo bora ya kusuluhisha haraka tofauti na migogoro ya kibiashara na uwekezaji. Kwa ajili hiyo, tumeimarisha Mahakama Kuu, Kitengo cha Biashara au Mahakama ya Biashara kama inavyojulikana, pia tumeanzisha Kitengo Maalum cha Kusikiliza Malalamiko ya Uwekezaji *(Investors Compliance Beaurea)* chini ya Ofisi ya Katibu Mkuu Kiongozi, ili kudhibiti na kusimamia viwango vya huduma na bidhaa, tumeimarisha Tume ya Ushindani wa Haki wa Kibiashara, Wakala wa Chakula na Madawa na Shirika la Viwango. Vyote hivi ni vyombo vinavyotusaidia katika kutengeneza mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kutambua ushiriki wa sekta binafsi katika masuala ya ubia, Serikali imeandaa Sera ya Ubia na jana Bunge lako Tukufu limepitisha Muswada wa Sheria wa Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Nawashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge, lengo letu ni kuweka bayana mfumo wa utaratibu utakaowezesha kuwepo ushirikiano kati ya sekta binafsi na sekta ya umma, kila mmoja anamuhitaji mwenzake. Kabla ya hapo, hatukuwa na utaratibu unaoeleweka, sasa tumeweka utaratibu naamini itatusaidia sana kukuza uwekezaji na kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli mbalimbali za Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, tumeendelea kuimarisha majadiliano kati ya Serikali na Sekta Binafsi, Mabaraza ya Biashara ya Mikoa na Wilaya yamekwishaundwa kwa ajili ya kuboresha mazingira ya uwekezaji na kuibua fursa za uwezeshaji kiuchumi wa wananchi. Tumeendelea kuchukua hatua za kisera na kisheria kwa lengo la kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara nchini. Shabaha yetu ni kuona uwekezaji unaendelea kuongezeka nchini kama ilivyotokea kati ya mwaka 2005 na 2008. Uwekezaji umekua kutoka dola 568 milioni na kufikia dola 744 milioni mwaka 2009. Siyo kiasi kidogo, lakini mwaka jana ulishuka ukawa dola 550 milioni na kielelezo chake ni kama nilivyoeleza ni kwa sababu ya kudorora kwa uchumi wa dunia, wale waliokuwa na nia ya kuwekeza nao pia wamepunguza kasi.

Mheshimiwa Spika, uwezeshaji wa wananchi, ni moja ya dhima kuu ya Ilani ya Uchaguzi wa Chama chetu. Tuliahidi kuwa, Serikali itaendeleza mifuko ya uwezeshaji. Tumeimarisha mifuko hiyo, tuna Mfuko wa Vijana, Mfuko wa Akinamama, Mfuko wa Kuwawezesha Wajasiriamali Wadogo Wadogo *(Small Enterprises Loan Facility*

(SELF)), Mfuko wa Dhamana ya Mikopo kwa Wafanyabiashara Wadogo. Tumeanzisha Mfuko wa Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi maarufu kama Mabilioni ya Bwana Fulani, Watanzania hodari kweli. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kama tulivyoahidi kwenye Ilani, tumechangia sehemu kubwa ya mtaji wa mwanzo wa uanzishaji wa Benki ya Wanawake ambao tayari imekwishaanza. Wakati Mfuko wa Akinamama umekopesha zaidi ya wanawake laki tatu hadi Mei, 2010, Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi umekopesha shilingi bilioni 45.2 na zaidi ya wajasiriamali 67,000 wamenufaika. Halmashauri za Wilaya nazo haziko nyuma, zimekopesha vijana shilingi bilioni 1.16.

Mheshimiwa Spika, mipango ya Serikali ya uendelezaji wa sekta binafsi, uwekezaji na uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, imewezesha shughuli za kiuchumi kupanuka na hivyo kuchochea ongezeko la ajira nchini. Hivyo, utekelezaji wa ahadi ya Ilani ya Uchaguzi kuhusu kuzalisha ajira milioni moja umekwenda vizuri. Hadi kufikia Juni, 2010, ajira 1,313,121 zilikuwa zimezalishwa lakini bado tatizo la ajira ni kubwa na kazi hii lazima tuifanye zaidi, ya kuhakikisha kwamba vijana wetu wengi na hata watu wazima wanaendelea kuingia kwenye fungu la kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, vilevile tumetimiza ahadi yetu ya kuimarisha ushirika nchini kama nguzo kuu ya kuunganisha nguvu za wanyonge kujiletea maendeleo. Chini ya uongozi wetu, idadi ya Vyama vya Ushirika nchini vimeongezeka kutoka 5,730 mwaka 2005 imefikia 9,501 mwaka huu. SACCOs zimeongezeka kutoka 1,875 mpaka 5,344. Akiba na amana kwenye dhamana za wanachama zimeongezeka kutoka bilioni 31 mpaka bilioni 174.6. Kwenye nishati ya wananchi wenyewe, wakijipanga vizuri, fedha wanazo mikononi mwao, mkizitengenezea utaratibu, zinaweza zikatoka na zikafanya kazi ya kuwasaidia kuinua hali zao za maisha.

Mheshimiwa Spika, kuna Vyama vya Ushirika 38 vilikuwa vinadaiwa shilingi bilioni 26.8. Sisi katika Serikali, tuliamua kubeba mzigo huo wa madeni ili tuviwezeshe kupata mikopo, vyama hivyo sasa vinakopeshwa. Rai yangu ni kwamba, wahakikishe hawarudi tena kwenye madeni, wahakikishe kwamba wale wezi waliovifikisha mahali vyama hivyo vikawa na madeni makubwa, hawapewi tena nafasi za uongozi ili tusirudi kwenye matatizo yale ya zamani. Nilikwenda mahali wakaniomba niwasaidie kukinusuru Chama chao, nikasema hamuwezi kuiba nyie, tutumie hela za walipa kodi kukinusuru Chama chenu, shauri yenu, lakini baadaye tuliwasaidia kwa kubeba yale madeni.

Mheshimiwa Spika, tuliahidi kwamba tutaendeleza sekta ya kilimo, tulianzisha Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo *(ASDP).* Programu hiyo, kazi yake ilikuwa ni kutoa msukumo wa kuendelea kuleta mageuzi ya kilimo nchini. Bajeti ya kilimo tumeiongeza kutoka shilingi bilioni 233.3 mwaka 2005 katika bajeti ya mwaka huu imefikia bilioni 903.8. Bado hatujafikia asilimia 10, lakini ndugu zangu safari ni hatua, tulitoka kwenye bilioni 233 sasa tuko bilioni 908 ambayo ni sawa na asilimia 7.8, asilimia 10 tutafikia tu.

Mheshimiwa Spika, katika miaka mitano iliyopita, tumetimiza ahadi niliyoitoa hapa Bungeni ya kuhakikisha kuwa upatikanaji na matumizi ya pembejeo kwa wakulima vinaongezeka. Tumeongeza fedha kwenye Mfuko ya Ruzuku ya Pembejeo kutoka shilingi bilioni 7.5 mwaka 2005 hadi shilingi bilioni 143.8 mwaka huu na matokeo yake ni nini? Wakulima wengi zaidi wanapata mbolea, wanapata mbegu bora na kwa hiyo tija inaongezeka na safari yao ya kujiondoa kwenye lindi la umaskini, linaonekana kuwa ni la uhakika.

Mheshimiwa Spika, tumeimarisha vituo vya utafiti wa kilimo kwa nia ya kuongeza kujihakikishia kwamba tunapata mbegu za kutosha. Mwaka huu, tumetenga shilingi bilioni 30 kwa ajili ya shughuli za utafiti na vilevile vituo vya kilimo vitanufaika. Tumechukua hatua za kuongeza uwezo wetu wa kuzalisha mbegu hapa nchini, tumefufua mashamba yetu ya mbegu, tumeanza kufahamu mashamba yetu ya mbegu lakini pia niliagiza Jeshi la Magereza na Jeshi la Kujenga Taifa vishiriki katika kuzalisha mbegu nchini. Hivi sasa asilimia 75 za mbegu tunatozumia nchini tunaagiza kutoka nje. Tumeanza safari ya kupunguza utegemezi huo, uzalishaji wa mbegu umeongezeka kutoka tani 10,000 mwaka 2005 tumefikisha tani 16,144.79 Desemba mwaka 2009 na kadri tunavyoendelea, tutaendelea kuongeza zaidi uwezo wetu.

Mheshimiwa Spika, tumesema tutahakikisha pia usambazaji wa mbegu bora unakuwa rahisi na mbegu zinawafikia wakulima kwa bei nafuu. Tumeimarisha Wakala wa Mbegu wa Serikali (*Agricultural Seed Agency*) kwa ajili ya kusimamia uzalishaji wa mbegu kwa wingi na kuhakikisha kwamba mbegu zinasambazwa kwa urahisi na kuwafikia walengwa.

Mheshimiwa Spika, katika miaka mitano hii tumeanza kuchukua hatua za polepole kuanza kubadilika kutoka kutegemea jembe la mkono na kuanza kuelekea sasa kutumia mashine katika kilimo chetu, zana bora, kwa sababu hiyo tumeendelea kutoza ushuru kwa matrekta ambapo matrekta 1,737 yameingizwa kati ya mwaka 2006 na 2009. Unaweza kuona bado ni kidogo lakini katika kipindi hiki ni mengi zaidi kulikoni yaliyokuwa yanaingizwa huko nyuma, kwa mwaka unaingiza trekta 50, 10, 15 sasa angalau tumefikia hatua hiyo.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya matrekta yaliyoingizwa nchini yalinunuliwa kutokana na mkopo wa shilingi bilioni 16.3 kutoka Mfuko wa Pembejeo. Kwa ujumla Mfuko wa Pembejeo nao tumeuongezea fedha kutoka shilingi bilioni 4.9 mwaka 2005, mwaka huu tumeutengea shilingi bilioni 30 ili tuweze kuleta mageuzi katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, tunategemea kupata matrekta 3,000 mwaka huu, idadi hii ya matrekta inayoingizwa nchini, ni kubwa kuliko kipindi kingine chochote katika historia ya nchi yetu. Tumeimarisha huduma za ugani, tumeajiri wataalamu 1,802 wa kilimo katika Halmashauri ambao wanafanya kazi ya kuwapatia wakulima mafunzo juu ya ukulima wa kisasa. Katika mwaka 2009/2010, Halmashauri za Wilaya zimenunua matrekta 2,154 madogo na 53 makubwa. Serikali ilizitaka Halmashauri za Wilaya ziwe

chachu ya kuleta mapinduzi ya kilimo. Kwa hiyo, nao waagize matrekta wawauzie wakulima hasa kwenye vikundi vyao vya uzalishaji ili waanze kubadili kilimo chao.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mifugo, dhamira yetu ilikuwa kuboresha mifugo na ufugaji wetu tutoke kwenye ufugaji ili tuanze kuingia kwenye ufugaji wa kibiashara. Tulichokifanya ni nini? Kwanza, tumefanya shughuli za mifugo kuwa sehemu kamili ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo. Katika miaka mitano hii, tumehimiza utumiaji wa madume bora ili kuongeza ubora wa mifugo yetu. Nilijifunza kwamba ili uharakishe, tutumie uhamilishaji au kwa lugha ya Kiswahili kupandisha kwa chupa ama kwa Kiingereza *artificial insemination*, unajenga uwezo mkubwa sana. Tumehamasisha matumizi hayo. Pia Kituo cha Uhamilishaji kilichoko Usa River, Arumeru tumekiimarisha. Wakati mmoja nilikitembelea kituo kile, nikakuta wana matatizo ya vifaa fulani, nikawatafutia pesa, wakapata vifaa vile na sasa uwezo wao umekuwa mkubwa zaidi. Wameshaanzisha vituo vitano katika kipindi hiki vya kusambazia mbegu Dodoma, Mwanza, Lindi, Kibaha na Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeajiri Maafisa Ugani 1,500 kusaidia kuwaelimisha wafugaji juu ya ufugaji bora na kusaidia kutoa huduma za ushauri na kuboresha mifugo yao na ufugaji. Wafugaji hawa nao wamenufaika na ruzuku kwa kupata dawa za kinga na tiba kwa mifugo yao. Katika kipindi hiki, ng'ombe 11,130,000 wamechanjwa kinga ya homa ya mapafu. Tumetumia shilingi bilioni 13.5 kwa ajili ya dawa za majosho, majosho 543 yamejengwa, juhudi zinaendelea za kujenga malambo, mabwawa, visima ili kuipatia mifugo yetu maji ya uhakika. Vilevile juhudi za kuimarisha ranchi ya Taifa nayo inaendelea na mafanikio yake tunaanza kuyaona na viwanda vya kusindika nyama vimeanza kujengwa. Kwa nia ya kutoa msukumo maalum, nimeagiza tuanzishe Programu Maalum ya Kuendeleza Mifugo Nchini, *ASDP* ibakie na kilimo na tuanzishe ya mifugo peke yake.

Mheshimiwa Spika, niliahidi mwaka 2005, nitatoa kipaumbele kwa sekta ya uvuvi. Tumeunda Wizara, tumeitoa sekta ya uvuvi kutoka Maliasili ilipokuwa haitambuliki, tumeunganisha katika sekta ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Mtu mmoja siku moja akasema Wizara ya Kitoweo na ina Waziri mchangamfu kweli, anachemka kweli Mheshimiwa Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mavuno ya samaki yameongezeka kati ya mwaka 2009, tumeuza nje samaki wenye thamani ya shilingi bilioni 783. Katika jitihada tunazozifanya, shabaha yetu ni kwamba katika miaka ya mbele tutafanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika miaka mitano hii sekta ya viwanda iliendelea kustawi vyema, kasi ya ukuaji wa sekta hii ilikuwa nzuri. Ukichanganya viwanda na ujenzi, imekua kwa asilimia 8.8. Sekta ya uzalishaji viwandani, *manufacturing sector* imekua kwa asilimia 9.14 na viwanda vilivyochangia sana ni vya saruji, vifaa vya umeme na vinywaji, usindikaji wa nafaka na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tumechukua hatua za makusudi kuchochea uwekezaji, tumeanzisha Mamlaka ya Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje (*Export Processing Zone Authority*). Tumeanzisha Maeneo Maalum ya Kiuchumi (*Special Economic Zones)*, viwanda 28 vimeshajengwa katika hizo *EPZ* na kipindi hiki na mauzo nje yamekuwa dola milioni 235. Katika *SEZ* tunavyo viwanda 12 ambavyo hivi sasa vinaendelea kujengwa.

Mheshimiwa Spika, madini ni sekta yetu ya pili kwa kuingiza fedha za kigeni. Mwaka 2005 tulipata dola milioni 720, mwaka 2009 tumepata dola milioni 1,219 yaani 1.216 trilioni, toka 720, ni sekta kubwa, ni sekta muhimu sana. Ajira kwenye migodi imeongezeka kutoka 7,000 mpaka kufikia 13,000.

Mheshimiwa Spika, hivyo, kuendeleza uchimbaji ni moja ya malengo muhimu ya Serikali yetu. Miongoni mwa mambo muhimu ambayo tuliamua kufanya ni kuitazama upya mikataba ya madini, kuitazama upya Sera ya Madini na kuitazama upya Sheria ya Madini, nia yetu ni kuhakikisha kuwa uwekezaji katika sekta hii unaendelezwa kwa kasi nzuri lakini pia na wananchi wananufaika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, niliunda Kamati wakati ule chini ya aliyekuwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Masha kupitia upya mikataba ya madini. Wakafanya kazi nzuri na katika maoni ya mapendekezo yao, waligundua kwamba kuna kipengele kinaitwa nyongeza ya asilimia 15 kwenye mtaji wa awali ambao haujarejeshwa. Suala hili lingeendelea ni kwamba migodi hii ingemaliza madini bila ya kulipa kodi ya mapato. Kwa sababu imewalinda, tukasema hoja yetu ni kwamba kwa nini walindwe wawekezaji tu, tusilindwe na sisi wenye dhahabu? Maana analindwa huyu aliyekuja kuwekeza na hasara yake inalipwa kwa dhahabu yangu, nasema sasa biashara hii haiwezekani. Kwa hiyo, tukasema kwamba hapa kwa sababu ni mikataba yetu halali tuanze *negotiation*, tukafanya mazungumzo na Makampuni manne makubwa ya madini, nafurahi tumekubaliana. *(Makofi)*

Tumekubaliana kipengele kile kwenye Mikataba ile kiondolewe na faida yake ni nini? *Golden Pride* ya Nzega, *Geita Gold Mines* ya Geita, *Tanzanite One* wameanza kulipa kodi. Baadhi ya miradi ya *Barrick* itaanza kulipa kodi katika kipindi kifupi kijacho.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo tulilifanya ni kujenga uwezo wa ndani wa kukagua uzalishaji katika migodi ile. Tulikuwa hatuna uwezo huo, tukakodisha Kampuni ya Alex Stuart.

Baada ya Mkataba wao kwisha na tulipoamua tusiendelee nao tukaamua kuunda Wakala wetu wenyewe wa Kukagua uzalishaji katika migodi hii mikubwa. Wakala umefanya kazi nzuri ya kubaini gharama halisi za uwekezaji na shughuli zinazoendelea migodini ili kodi yetu iweze kulipwa. Kutokana na hatua hizi mbili, mchango wa Sekta ya Madini kwenye mapato ya Serikali nao umeongezeka. Mwaka 2005 Serikali ilikuwa inapata shilingi bilioni 457, mwaka 2008 tulipata bilioni 840. Naamini mwaka jana itakuwa imeongezeka zaidi na tukizipata tutaendelea kupata zaidi.

Mheshimiwa Spika, Novemba mwaka 2007 niliamua kwamba katika Kamati nijumuishe watu nje ya Serikali katika kazi iliyokuwa inafanywa na Kamati ya Ndugu Masha. Ndipo tukaunda Kamati ya Mheshimiwa Jaji Mark Bomani na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge mlikuwa ni Wajumbe wa Kamati hiyo.

Kamati imefanya kazi nzuri sana, imetoa mapendekezo mazuri, mapendekezo haya yametusaidia kutengeneza Sera mpya ya Madini na kutengeneza Sheria Mpya ya Madini. Napenda kutumia nafasi hii kutoa pongezi na shukrani zangu kwa Mheshimiwa Jaji Mark Bomani na Wajumbe wake wa Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya. Kwa Mheshimiwa Lawrence Masha na Wajumbe wake kwa kazi nzuri pia waliyoifanya. Tumeanza pia kuchukua hatua za kuwaendeleza wachimbaji wadogo na sasa tunatoa leseni za uchimbaji ili kuhamasisha wachimbaji wadogo na kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Utalii ndiyo ya kwanza kwa kuingizia mapato ya Kigeni katika Serikali yetu. Tuliamua kwa upande wa utalii tuendelee kujitahidi kuindeleza Sekta hii muhimu na hasa tuitangaze duniani kwenye masoko makuu ya watalii. Ni shughuli yenye gharama lakini faida yake ni kuongezeka kwa watalii. Nilisema wakati ule nilipokuja mara ya mwisho mwaka 2008 watu wakaitafsiri vibaya. Lazima utumie ili upate. Siku ile nilieleweka vibaya kweli, mnisamehe. Nilikuwa natafsiri Kikwere kupeleka Kiswahili. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na jitihada hizi watalii wameongezeka na mapato ya utalii yameongezeka kutoka shilingi bilioni 823 kwa mwaka 2005 hadi shilingi bilioni 1,198.76 kwa mwaka 2008. Mwaka 2009 mapato yakashuka kufikia shilingi bilioni 1,162.8 lakini yote ni kwa sababu ya kudorora kwa uchumi wa dunia ambapo watalii walipungua na wale wachache waliokuwa wanakuja walikuwa hawakai siku nyingi. Wamepunguza siku, kwa hiyo mapato yetu yakapungua.

Hivi sasa hali inaonekana kuanza kurejea kuwa ya kawaida. Hivyo tutegemee Sekta yetu hii kupanda tena na itaendelea kuwa ya kwanza. Maana ukiangalia kwa hesabu hizi madini sasa kwa mara ya mwisho imeizidi Sekta ya Utalii. Madini inatoa *1.2 trillion* na Utalii *1.1 trillion*. Lakini *cumulatively* katika miaka mitano hii Sekta ya Utalii ndiyo imetoa mchango mkubwa zaidi kuliko Sekta ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kujenga mazingira mazuri ya ukuaji wa uchumi, kuongeza uzalishaji, kuboresha maisha ya Watanzania kama miundombinu ya usafirishaji ni mibovu na haitoshelezi mahitaji. Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 ilituagiza kwamba ifikapo mwaka 2010 tuwe tumekamilisha kutekeleza miradi 17 ya Barabara Kuu.

Leo hii ninaposimama mbele yetu kati ya miradi 17, tumekamilisha miradi 12 na mitano iliyosalia ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Tumekamilisha barabara ya Singida – Shelui, Shelui – Igunga – Nzega, Nzega – Ilula, Muhutwe – Kagoma, Nangurukuru – Mbwemkuru – Mingoyo, Mkuranga – Kibiti, Pugu – Kisarawe, Chalinze – Morogoro –Melela, Tunduma – Songwe, Kyabakari – Butiama, Dodoma – Morogoro, Dodoma –Manyoni, Buzirayombo – Kyamyorwa, Buzirayombo – Geita.

Mheshimiwa Spika, ndani ya miaka hii mitano tumekamilisha ujenzi wa miradi ya barabara 26 zenye urefu wa kilomita 2,237. Sasa hivi tunaendelea na ujenzi wa miradi 28 yenye urefu wa kilomita 2,208. Lengo letu la kuunganisha Mikoa yote kwa barabara za lami lina mwelekeo mzuri.

Hivi sasa katika Mikoa ya Mtwara Lindi, Ruvuma, Rukwa Kigoma na Tabora kuna kazi za ujenzi wa barabara zinazoendelea mahali fulani au kuna mchakato wa kuanza kazi hiyo ambayo imefikia katika hatua ya utekelezaji ama Mkandarasi yuko kwenye *site* ama Mkataba umekwishatiwa saini, kinachosubiriwa ni kazi ile kuanza. Katika barabara za Mikoa kilomita 121 zimejengwa kwa kiwango cha lami, kilomita 1,979 zimefanyiwa matengenezo katika kiwango cha lami na kilomita 3,114 zimefanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki madaraja 8,385 yalifanyiwa matengenezo ya kuzuia uharibifu, madaraja 660 yamefanyiwa matengenezo makubwa, madaraja 53 yamejengwa likiwemo daraja ya Mpiji, daraja la Ruvu na daraja la Umoja linalounganisha Tanzania na *Mozambique*.

Daraja hili ni miongoni mwa urithi tuliorithi kutoka kwa Baba wa Taifa. Walikuwa na dhamira na Rais Samora na wote wametangulia mbele ya haki kwamba lijengwe daraja kwenye Mto Ruvuma liunganishe nchi zetu hizi mbili. Daraja hilo limekamilika na mwezi uliopita tumelifungua daraja hilo rasmi. Usanifu kwa baadhi ya madaraja umekamilika na kinachosubiriwa sasa ni pesa zipatikane ujenzi uanze.

Daraja ya Kilombero ni miongoni mwa madaraja haya. Tumenunua vivuko vipya vitano na kukamilisha ujenzi wa vivuko viwili na kazi inaendelea, ujenzi wa vivuko kadhaa. Nafurahi kwamba kero kubwa zilizokuwepo Kigamboni, hazipo tena, Busisi haipo tena, Pangani kwa jamaa zangu kule halipo tena, Kome kwa Mheshimiwa Chitalilo halipo tena tatizo hilo. Hivyo ni baadhi ya vivuko ambavyo vilikuwa kero kubwa na matatizo hayo tumeyamaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pesa nyingi tumezitenga katika Mfuko wa Barabara na kuzigawa kwenye Halmashuri zimesaidia kuimarisha barabara za Wilaya na Vijiji. Kwa ujumla jitihada na hatua zote hizo tulizochukua zimesaidia kuwezesha barabara nyingi nchini kupitika karibu mwaka mzima. Lakini bado kazi inaendelea. Nchi yetu ina barabara za urefu wa KM 85,000. Unajua kila kitu kina faida yake na hasara yake. Mkipata nchi kubwa hilo ndilo tatizo lake.

Sasa sisi Tanzania ni mara mbili *size* ya Kenya, watu hawajui hilo. Ni mara tatu *size* ya Uganda. Sasa tumesema hii kazi ya umeme ingekuwa nchi kama Malawi ile *Grid* tu kuitoa Kidatu ukaifikisha kule Tarime kama ni Malawi unaweza kupeleka umeme mpaka kwenye matendegu ya vitanda. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukipima hivyo ndipo utakapojua uzito wa kazi tuliyokuwa nayo sisi. Maana wakati mwingine watu wanatembelea nchi ndogo ndogo wakirudi wanasema nilikwenda Malawi, mambo mazuri kweli, barabara zote za lami. Jamani sisi

nchi yetu hii, *is a giant country*. Kwa hiyo, ukubwa wake ni tatizo. *Investment* hizi tunazozifanya sisi kwa kweli ni pesa nyingi tunazozitumia, ingekuwa ni nchi yetu ni ndogo ingekuwa kila mahali umeme upo, maji yapo, barabara zipo kila kitu kipo. Lakini hatulalamiki kupewa nchi kubwa. Ni changamoto ya kuongeza juhudi na maarifa ili tufanye maisha ya watu wetu kuwa mazuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nyote ni mashahidi kwamba tumehangaika sana na reli zetu mbili, *TAZARA* na Reli ya Kati katika kipindi hiki cha miaka mitano. Kwa miaka kadhaa, reli zetu hizi zilikuwa na matatizo mengi na kusababisha huduma za uchukuzi wa abiria na mizigo kuathirika. Kiini cha matatizo ni uendeshaji usioridhisha na huu tumeanza nao sisi wenyewe.

Sisi tulipokuwa na matatizo ya kuendesha treni zinaishia Dodoma na zinaanzia Dodoma, ndipo ikatokea dhana kwamba labda tupate Kampuni ya uendeshaji. Ikapatikana Kampuni ya *RITES* ilianza katika kipindi cha Awamu ya Tatu, sisi tukaja katika hatua za mwisho wakati huo tuliamini kwamba itasaidia kupata jawabu kwa tatizo linaloisibu reli yetu.

Bahati mbaya matarajio yetu hayakuwa hivyo. Tumefanya uamuzi mgumu, tumesema tunawashukuru sana, lakini tuachane tuanze upya. Tuichukue wenyewe halafu tupange namna ya kuanza upya katika njia bora zaidi ya kuendesha reli yetu. Mazungumzo yanaendelea sasa hivi juu ya kuwalipa haki zao ili tuseme *thank you, good lucky*. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *TAZARA* nayo matatizo ni hayo hayo. Ilifika mahali pale wamechukua hela za watu, wanashindwa kusafirisha mizigo. Matatizo yakabaki pale pale ya uendeshaji. Nalo tumekuwa tunaendelea kuhangaika nalo. Mazungumzo yetu sisi na Zambia, tumewajumuisha na wabia wetu, tumejaribu kutafuta majawabu ya uendeshaji kwenye reli zetu hizi. Niseme tu kwamba ni dhamira yetu kwa kweli, kutafuta jawabu ili viungo na miundombinu hii muhimu kwa uchumi wa nchi yetu iweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miaka mitano hii nishati ilikuwa na changamoto kubwa. Tulikabiliwa na tatizo kubwa la upungufu wa umeme kwa sababu ya ukame hakuna haja ya kurudia tena. Lakini tukajifunza tupunguze kutegemea sana umeme wa maji na bahati nzuri Mwenyezi Mungu ametujalia vyanzo vingi. Tuna makaa ya mawe, tuna gesi asilia, kuna upepo mwingi, kuna jua kali lakini pia kuna madini ya *Uranium*.

Kwa utafiti uliofanyika pale Namtumbo peke yake pale kuna mashapo *reserve* ya *pounds* milioni 90 na kwa *pounds* milioni 90 Tanzania ni ya saba kwa kuwa na *Uranium* nyingi duniani. Utafiti bado unaendelea wako Bahi, wako Manyoni na kwingineko tunaweza tukazidi hapo. Kwa hiyo, vyanzo vya kuweza kuzalisha nishati tunavyo. Tukaamua tuanze kuelekea huko. Hivi sasa tumeongeza uzalishaji wa umeme kutokana na gesi asilia kwa *Megawatt 145*. Tuna mtambo mpya pale Ubungo wa *Megawatt* 100, tuna mwingine kule Tegeta wa *Megawatt* 45.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa mchakato unaendelea wa kuongeza mtambo mwingine wa *Megawatt* 100 pale Ubunge na mtambo mwingine wa kutumia mafuta wa *Megawatt 60* kule Mwanza. Bahati mbaya mpango wetu wa kuzalisha *Megawatt 300* pale Mtwara ukakumbwa na msukosuko wa uchumi duniani. Wawekezaji tuliopatana nao wakashindwa kupata mikopo na kwa hiyo, mradi ule umesimama.

Lakini sasa hivi tuna mazungumzo na wabia wawili wengine na tunajaribu kutafuta vyanzo vya kupata mikopo ili tutengeneze ule mradi. Tulikusudia umeme wa *Megawatt 200* kutoka Kiwira, haukuweza kupatikana kutokana na matatizo ya milki ya mgodi ule wa Makaa ya Mawe wa Kiwira. Matatizo hayo tumeyamaliza na kwa hiyo, nao sasa tunaendelea pia kutafuta vyanzo mbalimbali, tunaamini uzalishaji huo utaanza. Tukipata Megawatt hizo 500, nina hakika tutakuwa tuko mbali.

Mheshimiwa Spika, tarehe 12 Juni, Bunge lako lilitunga Sheria ya Umeme Na. 10 ambayo imetoa fursa pana zaidi kwa sekta binafsi kushiriki katika uzalishaji na usambazaji wa umeme nchini. Utaratibu huu mpya umepata mwitikio mzuri na sasa tayari wako wawekezaji binafsi wanne ambao wako tayari kuzalisha umeme na kuiuzia *TANESCO*.

Ninaamini katika miaka mitano ijayo wawekezaji kutoka Sekta binafsi wataongezeka na hivyo kulihakikishia taifa letu umeme wa uhakika. Katika miaka mitano hii tumefanikiwa kuyapatia umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Serengeti, Ukerewe, Mbinga, Simanjiro, Ludewa, Mkinga, Kilolo, Uyuwi, Kilindi na Bahi.

Mipango ya kuzipatia umeme Wilaya za Bukombe, Longido, Ngorongoro, Kasulu, Kibondo na Nkasi iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kama isingekuwa kuongeza zile Wilaya nyingine karibu 20 tungesema kwamba suala la umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya limekwisha. Lakini tumejiongezea mzigo lakini mzigo wenyewe wa kheri. Ni mzigo wa kuleta maendeleo ya Watanzania na Wilaya hizo nazo tutaubeba mzigo wake zile ambazo hazina umeme tutapaleka umeme kwa sababu ni sera rasmi ya Serikali kwamba kila Makao Makuu ya Wilaya yapate umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi hiki pia tumeendelea na jitihada za kuunganisha Mikoa ya Ruvuma, Kigoma, Kagera na Rukwa kwenye *Grid* ya Taifa. Tumekamilisha taratibu kwa Mkoa wa Ruvuma, tumepata mkopo kutoka Sweden, tulikuwa tunajadiliana juu ya kiwango cha riba lakini hatimaye sasa tumeshaelewana.

Kwa hiyo, kwa ile iliyobakia ni kazi kuanza, mwelekeo wetu sasa wa kuanzia Shinyanga kuupeleka umeme kwanza Kagera halafu ukate pale Nyakanazi uingie Kakonko, Kibondo, Kasulu Kigoma halafu ukate kule Uvinza uingie Mpanda, Sumbawanga mpaka Tunduma nao tunaendelea hivi sasa. Tumefika mahali hatuwezi kusema kwamba ni mahali pazuri sana lakini sio pabaya pia kwa sababu mazungumzo yameanza na mwelekeo unaelekea kuwa ni mzuri.

Mheshimiwa Spika, katika miaka mitano hii, mwaka 2007 tulianzisha Wakala wa Umeme Vijijini. Umefanya kazi nzuri katika kipindi chake kidogo cha miaka mitatu.

Kasi ya upelekaji umeme vijijini imeongezeka na kasi kubwa ya kupeleka umeme kwenye Wilaya ni kitu kinachotokana na kazi nzuri ya *REA*. Vijiji 180 vimepatiwa umeme, shilingi bilioni 9.4 zimetumika kwa ajili hiyo na kazi inaendelea. Tutakavyokwenda kuimarisha zaidi tutapata mafanikio zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ardhi na makazi, nako tumepiga hatua. Kati ya Januari, 2006 na Mei, 2010 tumefanikiwa kupima na kutoa hati kwa vijiji 6,129. Idadi hii inafikisha vijiji 10,682 vilivyopimwa kati ya vijiji vyetu 11,000. Tumeshapima asilimia 97 ya vijiji vyetu. Mtakubaliana nami kwamba haya ni mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile tumeendelea na mipango ya matumizi ya ardhi, kupima mashamba ya wanavijiji na kutoa hati miliki za kimila. Jumla ya hati miliki 54,395 zilitayarishwa na kutolewa kwa wananchi katika Wilaya za majaribio. Tumeanza na Mbozi, Babati, Bariadi, Namtumbo na Manyoni. Kule Wilaya ya Mbozi wakulima wamezitumia hati hizo kwa kukopea na wamepata mikopo ya yenye jumla ya shilingi bilioni 10.38 kwa kutumia hati hizi za kimila kama dhamana. Hii ni habari njema kwa upande wa uwezeshaji wa wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Januari, 2006 – 2010 tumepewa viwanja 37,458 katika maeneo ya miji mbalimbali. Ili kuharakisha utoaji wa viwanja, Kanda sita za ardhi zimeanzishwa nchini ili mtu asilazimike kuja mpaka Dar es Salaam ndio apate hati ya kumili. Vile vile chini ya Programu ya MKURABITA ambayo Mwenyekiti wake wa Bodi ni Naibu Spika, nyumba 290,000 katika miji ya Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma, Tanga na Moshi zilitambuliwa na wamiliki wake kupewa leseni za makazi ambazo nazo ni sawa sawa kama hati nyingine zozote zile. Wanaweza kuzitumia nazo kama dhamana kukopea. Hii nayo ni uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika miaka mitano hii tumeboresha mazingira ya kuendeleza sekta ya mawasiliano nchini. Ujenzi wa Mkongo wa Taifa ulioanza Februari mwaka jana unaendelea vizuri. Kama kila kitu kitakwenda sawa, ifikapo Juni mwakani Makao Makuu ya Wilaya zote, Makao Makuu ya Mikoa yote yatakuwa yameunganishwa kwenye Mkongo wa Taifa.

Katika kipindi hiki, simu za mkononi zimeongezeka kutoka milioni 3.5 kufikia milioni 16. Tanzania ni ya pili Afrika baada ya Nigeria kwa kasi kubwa ya kuongezeka kwa matumizi ya simu za mkononi. Kila mtu yuko *connected*. Ni matumaini yangu kuwa katika siku za usoni, watumiaji wa simu za mkononi wataongezeka zaidi. Mkongo utakapokuwa umesambaa, utapunguza sana gharama za upigaji wa simu na kwa hiyo, watu wengi watakuwa na uwezo wa kumudu matumizi ya simu za mkononi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuipeleka nchi yetu katika Karne ya 21, tumeanzisha Mpango wa Kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika kuendeleza Elimu nchini. Mpango huo tunauita Tanzania *Beyond Tomorrow* (Tanzania Baada ya Kesho). Uko chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Tumeunganisha makampuni ya teknoloji hii ya mawasiliano makubwa ya Kimarekani; *Microsoft, IBM, CISCO, ACCENTURE, INTEL*. Ni mafanikio makubwa kuyakusanya makampuni yanayoshindana, kushirikiana pamoja kutengeneza mradi huu kwa ajili ya Tanzania. Utatuwezesha kutumia kompyuta katika kufundishia na kuwawezesha vijaa wetu kupata elimu. Mpango huo ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi. Hivyo, tutafanya kila tuwezalo ufanikiwe.

Mheshimiwa Spika, mara tulipoingia madarakani, ili kuhakikisha tunaongeza upatikanaji wa maji mijini na vijijini, tukaanzisha Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji inayotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano mitano kuanzia mwaka 2007 mpaka mwaka 2025. Utekelezaji wa Programu hii umetuwezesha kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama vijijini kutoka asilimia 53.7 mwaka 2005 hadi aslimia 60.1 mwaka 2010. Kwa mijini tumefikia asilimia 84 kutoka asilimia 74 mwaka 2005.

Katika kipindi hiki tumefanikiwa kukamilisha ujenzi wa mradi mkubwa wa upelekaji maji Shinyanga na Kahama kwa kutumia fedha zetu wenyewe na wananchi wapatao 1,000,000 wananufaika. Aidha, tumefanikiwa kuziwezesha Mamlaka za Maji katika Manispaa 13 kati ya 19 zilizopo kujitegemea kwa gharama zote za uendeshaji na matengenezo. Hawategemei tena bajeti ya Serikali, wao wenyewe sasa wanajiendesha na ndilo lengo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo letu la kufikia asilimia 65 vijijini na asilimia 90 mijini itakapofika mwishoni mwa mwaka huu bado hatutalifikia. Lakini, ipo kazi inayoendelea katika mwaka huu wa tano wa bajeti yetu, maana bajeti yetu ya kwanza mwaka 2006, ya pili 2007, ya tatu 2008, ya nne 2009 na ya mwaka huu ndiyo bajeti yetu ya tano kwa maana ya kipindi cha miaka mitano. Zipo kazi zinazoendelea, watatusogeza mahali. Lakini, lile lengo letu la asilimia 65 vijijini na asilimia 90 mijini hatutalifikia, tutakuwa pungufu kwa kiasi fulani. Yaliyobakia, tutayafanya katika miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Spika, maisha bora kwa kila Mtanzania ni pamoja na watu kuwa na afya bora. Katika kipindi hiki tulitunga sera mpya, tukatengeneza Mpango wa Miaka Kumi wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) kwa ajili ya kutekeleza sera hiyo. Mpango huu una malengo makuu yafuatayo:-

(Lugha za Bunge siku hizi zinanikwepa mimi). Ya kwanza ni kusogeza huduma za afya karibu na wanapoishi wananchi, hivyo, ujenzi wa Zahanati na Vituo vya Afya vijijini na kwenye Kata ni sehemu ya mpango huu. Hospitali za Wilaya na Mikoa ziboreshwe ili matatizo mengi ya afya yaweze kushughulikiwa huko.

Hospitali za Mikoa tumesema tunataka ziwe ndiyo Hospitali za Tufaa. Pili, kuongeza watalaam wa afya wa kazi zote kwa maana ya kupanua fursa za mafunzo na ajira. Tatu; kuboresha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na mahitaji mengineyo. Nne, kuongeza nguvu katika kupambana na maradhi hasa yale yanayoua na kusumbua watu wengi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, bajeti ya Sekta ya Afya tumeiongeza kutoka shilingi bilioni 271 mwaka 2005 hadi kufikia shilingi bilioni 1,205 mwaka huu. 271 kufikia trilioni 1.205, yaani kutoka asilimia sita ya bajeti kufikia asilimioa 10. Sekta ya afya tumeitoa kuwa ya sita, sasa ni ya tatu baada ya elimu na miundombinu. Kazi bado inaendelea kwa sababu tunataka tufikie kwenye lengo la asilimia 15 ya bajeti. Zahanati 1,403 zimejengwa, vituo vya afya 167, hospitali 24. Hospitali zote za Wilaya zimepatiwa *X-Ray* na *Utra Sound*, isipokuwa Wilaya saba ambazo nazo utaratibu wa kuzipatia unaendelea. Karibu hospitali zote za Mikoa zina maabara za kisasa na kwa msaada mkubwa wa *Abort Fund* tunaendelea kuziboresha zaidi.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wa taaluma mbalimbali za afya wameongezwa kutoka 1,059 kufikia 4,422 mwaka huu. Madaktari Bingwa wameongezeka kutoka 46, sasa tunao 265. Chuo Kikuu cha Dodoma kimeanza kufundisha Madaktari na mkakati wa kujenga Chuo Kikuu kipya pale Mloganzila karibu na Dar es salaam nao umeanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfumo wa upatikanani wa dawa nao umeboreshwa. Hivi sasa vituo vinapata dawa kwa mahitaji yake. Tumeongeza mapambano dhidi ya malaria na UKIMWI kutokana na nyongeza ya kupatikana vyandarua kwa watoto wa chini ya umri wa miaka mitano, kwa akina mama wajawazito kwa hati punguzo, matumizi ya dawa mseto.

Vifo kutokana na malaria vimepungua kutoka 80,000 na 100,000 mwaka 2005, sasa tuko 40,000 na 50,000 hivi sasa, imepungua kwa nusu. Sasa tunaendelea na mkakati wa kutokomeza malaria na mkakati wa kumuua mbu anayesabisha watu kupata malaria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeongeza sana uhamasishaji wa wananchi kujikinga dhidi ya UKIMWI. Tumeanzisha kampeni ya upimaji wa hiari ambayo imeitikiwa vizuri sana, hivi sasa watu milioni 11 wamekwishapimwa Tanzania. Maambukizi ya UKIMWI yamepungua kutoka asilimia 7.7 hadi asilimia 5.6. Haya sio mafanikio madogo, lakini hata watu watano katika kila watu 100 ni wengi mno. Hata mtu mmoja katika watu 100 kufa kwa UKIMWI ni wengi mno. Shabaha yetu ni kufikia mahali, hakuna mtu anayeambukizwa UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya kuzindua Bunge, aah, lakini hata kabla ya hapo, kuna sentensi nimeruka. Katika hotuba yangu ya kuzindua Bunge niliahidi kwamba tutaongeza jitihada za kupunguza kupeleka nje wagonjwa kwa ajili ya tiba. Tumeanza kazi ya kujenga uwezo wetu wa ndani kwa maradhi ya saratani, maradhi ya moyo na figo. Hivi sasa tumejenga uwezo wetu wa ndani na tunaendelea kuukuza uwezo huo ili tuunguze wagonjwa tunaowapeleka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipofungua Bunge, kuhusu elimu nilisema hakuna Taifa lililopata maendeleo bila ya kuendeleza elimu. Hivyo, kuendeleza elimu nchini itakuwa agenda muhimu ya Serikali ya Awamu ya Nne. Nasimama mbele ya Bunge hili nikiwa na faraja kubwa kutokana na mafanikio makubwa tuliyoyapata kwenye sekta ya elimu

nchini. Tumepanua elimu ya ya awali na msingi. Wanafunzi wa awali wameongezeka kutoka 638,591 mwaka 2005 hadi 825,465 mwaka 2010.

Shule za msingi zimeongezeka kutoka 14, 257 hadi 15,816. Wanafunzi wameongezeka kutoka 7,451,000 hadi 8,419,305 katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa asilimia 67 ya watoto wanaostahili kupata elimu ya msingi, wameandikishwa na uwiano wa kijinsia umezingatiwa. Mvulana mmoja, msichana mmoja. Tumeajiri walimu wapya 6,028 katika shule za awali. Tumeajiri walimu 49,694 wa shule za msingi. Aidha, nyumba za walimu 15,394 zimejengwa katika miaka minne hii, za sekondari na msingi pamoja.

Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na wananchi katika kipindi cha miaka mitano hii, tumeweza kujenga Shule za Sekondari 2,171 ukilinganisha na 1,202 zilizojengwa toka uhuru. Lengo la sekondari moja kwa kila Kata karibu tunalifikia, na zipo Kata nyingine zina sekondari zaidi ya moja. Sekondari binafsi zimeongezeka kutoka 531 kufikia 856 katika kipindi hicho.

Ongezeko hili limewezesha idadi ya wanafunzi wanaosoma sekondari kuongezeka kutoka 524,325 mwaka 2005 hadi kufikia 1,638,669, ongezeko la karibu mara tatu. Aidha, idadi ya wanafunzi wanaosoma Kidato cha Tano imeongezeka kutoka 9,710 na kufikia 33,169. Pia tumeajiri walimu wapya wa sekondari 14,329. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, 2006 – 2010, kwa kushirikiana na wananchi tumefanya upanuzi mkubwa wa sekondari. Lakini, upanuzi huo umezaa changamoto nyingi hasa za upungufu wa walimu, upungufu wa vitabu, vifaa vya kufundishia na nyumba za walimu.

Kwangu mimi hizi ni changamoto za maendeleo, maana mnaweza kuwa na changamoto za kutokuwa na maendeleo. Kwa sababu mmejenga shule nyingi, sasa mnaanza kutambua kwamba kunahitajika hiki na hiki. Kuna mipango thabiti na inayoendelea kutekelezwa kukabili kila moja ya changamoto hizo.

Mheshimiwa Spika, upanuzi wa mafunzo ya walimu katika Vyuo Vikuu umeongeza walimu wanaohitimu kutoka 500 mwaka 2005 kufikia 5,333 mwaka wa jana. Mwaka huu *UDOM* itaanza kutoa walimu, tutazidi kuendelea kupunguza pengo hilo.

Mheshimiwa Spika, tumeanzisha mpango kabambe wa kukabili matatizo ya vitabu, vifaa vya kufundishia, maabara na nyumba za walimu. Nyongeza kubwa ya bajeti ya Serikali kwenye elimu, ina shabaha ya kutoka bilioni 669 mwaka 2005 hadi kufikia bilioni 2,045 mwaka huu. Ni ushahidi tosha wa utashi wa kisiasa wa Serikali wa kuboresha elimu yetu nchini. Naamini katika miaka michache ijayo, matatizo yatapungua sana na mengine yatakuwa yamekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika miaka mitano hii, tumeshuhudia upanuzi mkubwa wa elimu ya juu nchini. Azma yetu ya kujenga Chuo Kikuu kipya imetimia, tena kwa mafanikio makubwa. Chuo Kikuu cha Dodoma kimeanza na ujenzi wa majengo ya Chuo hicho unaendelea kwa kasi kubwa.

Kila ukiangalia, kuna maghorofa tu yanajengwa kule. Chuo hiki ni fahari ya nchi yetu kwani tumekibuni wenyewe na tumekijenga wenyewe kwa kutumia fedha zetu, hatujapata msaada kutoka kwa mtu yeyote nje. Lakini wakiwa tayari kutusaidia waje. Pesa zetu tunazowekeza pale zitafanya shughuli nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika miaka mitatu ya mwanzo ya Chuo hicho tayari wameshafikisha wanafunzi 15,000 sina wasiwasi kabisa lengo la kufikia wanafunzi 40,000 litafikiwa ifikapo mwaka 2015, idadi ya wanafunzi wanaosoma Vyuo vya Elimu ya Juu vya Umma na Binafsi imeongezeka mara tatu katika kipindi cha miaka hii mitano kutoka 40,000 kufikia 117,068 katika kipindi hiki fedha za mikopo ya wanafunzi zimeongezeka kutoka bilioni 56 mwaka 2005 hadi 197.3 mwaka jana na mwaka huu tumefikisha bilioni 237.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wanaonufaika wameongezeka kutoka bilioni 16,345 hadi 69,981. Tumeanza kuchukua hatua za kurekebisha kasoro katika utoaji wa mikopo kupitia bodi ya mikopo na tunajaribu kutafuta utaratibu bora zaidi utakaorahisisha watu kupata mikopo ili mtu yeyote anayetaka kukopa akopeshwe bora awe tayari kulipa, niliahidi kwamba tutafanya jitihada kubwa kuhifadhi mazingira kwa ajili ya maendeleo endelevu ya nchi yetu niliunda Kamati ya Mazingira ya Baraza la Mawaziri chini ya Uenyekiti wa Makamu wa Rais nilitoa maelekezo kadhaa kuhusiana na uboreshaji wa mazingira kwa Wizara, Halmashauri za Wilaya na Miji kutekeleza, nafurahi maelekezo hayo hususan yahusuyo mifuko ya plastiki yaani mifuko ya rambo na kutunza vyanzo vya maji yametekelezwa na yanaendelea kutekelezwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla muamko wa wananchi wa kuhifadhi mazingira unazidi kukua tumefanikiwa kuiongezea Wizara hii uwezo na mamlaka ya usimamizi. Niliahidi kuendeleza shughuli za michezo na utamaduni na tumerudisha michezo mashuleni ili tujipe fursa ya kubaini vipaji vya watoto wetu mapema na kuviendeleza, nimetimiza ahadi yangu ya kugharamia mwalimu wa mpira wa timu yetu ya *Taifa Stars* kocha Marcio Maximo kutoka Brazil aliajiriwa na amesaidia sana kuinua kiwango cha soka hapa nchini. *(Makofi)*

Tanzania imepanda kutoka nafasi ya 172 mwezi Desemba, 2005 na kufikia nafasi ya 108 mmwezi Aprili mwaka huu na juzi hapa tumekuwa wa 112 baada ya mashindano ya Kombe la Dunia, mimi ninaamini hapa tulipofikia sasa tukiongeza juhudi zaidi tutapata mafanikio tunayoyatarajia, tumeshapata makocha wa riadha na ngumi nimekubali ombi la CHANETA kumlipia kocha wa netiboli wamtafute na Serikali itatafuta pesa za kumlipa, hatutaki watu watoe visingizio kuwa wamekosa mwalimu wa kufundisha tushindwe wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni nilisaidia kugharamia kambi ya mazoezi na posho ya wachezaji wa *Twiga Stars* maana nilikutana nao na waliniambia wanavunja kambi, nikawauliza tatizo lenu nini wakaniambia fedha. Nikawaambia wala msivunje kambi tutajikusuru kwani jungu kuu halikosi ukoko, tukatafuta pesa na timu ile iko kambini na kama hawakuiweka kambini matatizo yao wenyewe *TFF,* siyo ya pesa tunataka timu hii ambayo sasa imeshavuka vizuri iweze kushiriki mashindano ya wanawake ya soka Afrika. Ushindi wao ni fahari kwa nchi yetu ili waendelee kupeperusha bendera yetu vizuri. Nafurahi kwamba kupitia *Taifa Stars* moyo wa uzalendo umezidi kuongezeka miongoni mwa Watanzania tofauti na ilivyokuwa zamani, siku hizi ni jambo la kawaida kuwaona Watanzania wakivaa jezi za timu yetu ya Taifa na wakienda uwanjani wakiwa wanapeperusha bendera yetu ya Taifa, bado watu wanavaa za *Manchester*, za *Barcelona* lakini wakivaa na ya *Taifa Stars* nayo heri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sanaa hasa sanaa za maonyesho ambayo ni *music* na *film* katika miaka mitano hii tumeshuhudia kustawi sana kwa muziki wa kizazi kipya. Tumeshiriki kustawi kwa uigizaji wa sinema na Ze Komedi wamo humo, lakini ndugu zangu ninasikitishwa sana na hali ya wasanii wetu kutokupata malipo ya haki kwa kazi zao, niliamua kujaribu kusaidia nilipokutana na baadhi ya wasanii wa kizazi kipya wakanieleza haja ya wao kuwa na *mastering studio* yao ili waweze kumiliki kazi zao, niliwaambia watafute hiyo *mastering studio* watuambie gharama yake, tumeilipia dola milioni hamsini ambayo sasa wanayo *mastering studio* mali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakasema lipo tatizo lingine la namna ya kuuza kazi zao wamemtafuta wenyewe mshauri mwelekezi, wamempata Chuo Kikuu cha Dar es salaam, tumelipia shilingi milioni ishirini kwa ajili ya kazi hiyo ili tutengeneze njia bora ambazo wasanii wetu hawa wanaweza kusambaza kazi zao za muziki na filamu ili wapate malipo halali kwa jasho lao. *(Makofi)*

Ndugu zangu duniani kote huku hawa wasanii ni watu matajiri isipokuwa hapa kwetu wale kina Beyonce, Jay Z wanapata dola milioni 80 kwa mwaka, wacheza sinema wale wakubwa ni matajiri wakubwa lakini hapa kwetu ndiyo maskini kwa sababu hawamiliki kazi zao, kazi zao zinauzwa magendo sasa tutengeneze utaratibu utakaowawezesha wanufaike, mafanikio ya zoezi hili litatusaidia kufundisha namna ya kuwasaidia wasanii wa fani nyinginezo pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika miaka mitano hii tumepata mafanikio makubwa katika medani ya Kimataifa. Uhusiano wetu kiuchumi na kisiasa na mataifa na mashirika ya Kimataifa duniani umepanuka na kuimarika zaidi hakuna nchi yoyote duniani ambayo tunaweza kuita adui wa Tanzania haipo nchi rafiki na mashirika ya kikanda na Kimataifa yameendelea kuunga mkono jitihada zetu za kujiletea maendeleo, tumepata misaada mingi ya maendeleo katika kipindi hiki, tumepata misamaha ya madeni tunayodaiwa na kutupunguzia mzigo huu wa kuyalipa madeni haya, uwekezaji vitega uchumi kutoka nje umekuwa ukiongezeka kama nilivyosema, wigo wa masoko yetu ya nje umekua na unapanuka kwa bidhaa zetu, watalii kutoka nje wanaongezeka hakika diplomasia ya uchumi imetekelezwa kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, hadhi ya Tanzania katika nyanja za Kimataifa imepanda sana, tunasikilizwa, tunaaminiwa na tunathaminiwa. Kwa upande wa ajira katika Mashirika ya Kimataifa ndugu zangu hakuna mafanikio makubwa tuliyoyapata katika kipindi hiki kushinda yale ya Dada yetu Dr. Asha-Rose Migiro kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, ni heshima kubwa kwa nchi yetu, ni fahari kwa wanawake wa Tanzania hakika wanawake wakipewa fursa wanaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mimi ninafuatilia sana hakuna wakati wowote ninaokutana na Ban Ki-moon aache kumsifia Dr. Asha-Rose Migiro kwa jinsi anavyofanya kazi vizuri na lile dude kubwa la Umoja wa Mataifa; lina mikingamo mingi, lina mitego mingi na fitina nyingi lakini amefanya kazi zake vizuri na anaendelea kufanya kazi zake vizuri. Vilevile na wako Watanzania wengi kwenye mashirika mengi ya Kimataifa. Katika kipindi hiki pia tulibahatika kutembelewa na wageni wengi mashuhuri na wengine ni maajabu kututembelea. Tulitembelewa na Rais George Bush wa Marekani, amefanya ziara ya Afrika ya siku sita siku nne alikuwa Tanzania, Rais Hu Jintao wa China**,** Rais Abdullah Gul wa Uturuki, Rais Mary McAleese wa Ireland ambaye pia alipata fursa ya kuja kulihutubia Bunge hili kama vile alivyopata fursa ya kulihutubia Rais wa Comoro kuja kushukuru kwa msaada tuliowasaidia kuunganisha nchi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu wa zamani wa Ireland Bertie Ahern, Rais Innancio Lula da Silva wa Brazil, Waziri Mkuu wa China Wen Jiabao, Waziri Mkuu wa Canada Stephen Harper, Waziri Mkuu wa Norway Jens Stoltenberg, Malkia wa Denmark Margrethe II, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa na Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Dr. Asha-Rose Migiro maana msidhani kuwa alikuwa anakuja hapa nyumbani kwao, kuna ziara amekuja rasmi kama Naibu Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana mtu hawi nabii kwao, wanadhani huyu kaja kusalimia familia yake, hapana amekuja kikazi. Tumepokea Marais wengi wa Afrika kuja kututembelea yote haya yanadhihirisha ni kwa kiasi gani diplomasia ya Tanzania imefanikiwa sana. Tanzania imeendelea kushiriki vyema katika Umoja wa Afrika, katika *SADC* na Jumuiya ya Afrka ya Mashariki. Kwa upande mmoja Afrika tumepata heshima kubwa mwaka 2008 ya kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja huo, tulifanya kazi yetu vizuri kiasi cha kufanya baadhi ya viongozi wenzangu kufikiria tuendelee kwa mwaka mmoja zaidi nikakataa, nikasema kuwa tubaki na utaratibu wetu wa Mwenyekiti kukaa mwaka mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *SADC* tumeendelea kushiriki kwa ukamilifu katika shughuli zote za Jumuia hiyo ambayo inazidi nayo kuimarika. Jumuiya ya Afrika Mashariki katika miaka mitano hii tumeshuhudia utangamano ukizidi kuimarika na manufaa ya kiuchumi kwa Tanzania yakiendelea kushamiri. Umoja wa Forodha umefikia ukomo wake tarehe 1 Januari mwaka huu baada ya bidhaa kutoka Kenya nazo kuruhusiwa kuingia katika masoko ya nchi wanachama bila ya ushuru. Tarehe 1 Julai, 2010 Soko la Pamoja limeanza na matayarisho ya Umoja wa Sarafu nayo yameanza kupamba moto, Jumuiya ya Afrika Mashariki imekuwa na manufaa makubwa haya kiuchumi kwa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005 Tanzania ilikuwa inauza katika soko la Afrika Mashariki bidhaa zenye thamani ya dola milioni 161 mwaka 2008, tulifikisha milioni 353 na mwaka jana tukateremka tukafika 272 kwa sababu ya mtikisiko wa kiuchumi wa dunia. Ni kweli kwamba bado hatujatumia ipasavyo fursa zilizopo, tuendelee kujipanga vizuri kuna manufaa makubwa mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nimezungumza kwa muda mrefu sana, naomba nifikie mwisho, yapo mambo mengi muhimu ambayo ningependa kuyazungumzia mafanikio tuliyoyapata na changamoto tulizokumbana nazo lakini ninatambua kwamba wapo Waheshimiwa Wabunge wengi ambao wanataka kuwasha moto magari jioni hii hii kuwahi Majimboni, hivyo sitaki kuwaweka sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini kabla ya kumaliza hotuba yangu naomba kuwashukuru kwa kipekee viongozi wa nchi yetu waliotutangulia. Tumeendelea kuongoza nchi hii kwa mafanikio makubwa kwa sababu ya misingi madhubuti iliyowekwa na waasisi wa Taifa letu hili Mwalimu Julius Nyerere na Mzee Abeid Amani Karume na wataendelea kuwa ndiyo viongozi wetu. Pia natambua mchango mkubwa na msaada na ushauri wanaonipa Marais walionitangulia Mzee Ali Hassan Mwinyi na Mzee Benjamin William Mkapa ambao nao wakati wa uongozi wao waliendeleza juhudi za ujenzi wa Taifa letu kwa uwezo wao na umahiri waliojaliwa na Mwenyezi Mungu. Ninawashukuru sana kwa ushirikiano wao na msaada wao kwangu hawajavifunga visima vyao vya uzoefu, kila ninapotaka kwenda kuchota maji na kunufaika nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, ningependa kurudia shukrani zangu za dhati kwa Watanzania wenzangu wote, kwenu ninyi Wabunge hususani Spika wetu kwa kazi nzuri tuliyoifanya kwa kushirikiana katika mikutano iliyopita. Watanzania hatuna hulka ya kushikia bango la kusherehekea mafaniko yetu lakini kwa mafanikio tuliyopata katika miaka mitano iliyopita ukizingatia mazingira tuliyopitia, tuna kila sababu ya kujipongeza, naamini kabisa wananchi wanatambua, watatambua na watatuthamini sote tena na kutuongezea muda wakuendelea kuongoza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, wenzetu katika Mataifa mengine wanatuona kama mfano wa kuigwa Barani Afrika na wako tayari kutusaidia katika jitihada zetu. Hata hivyo tusibweteke kwa sifa hizo, bado kazi kubwa sana ipo mbele yetu, nina imani kabisa kama Mwenyezi Mungu akiendelea kutujalia na safari hii akatuepusha na majanga ya hali ya hewa na mengineyo na akabariki kazi za mikono yetu na akili zetu, tutapiga hatua kubwa zaidi na kwa kasi zaidi kuisukuma nchi yetu kwenye neema na watu wake kwenye maisha yaliyo bora, la muhimu kwetu ni kudumisha amani na utulivu. Tuendelee kupendana sisi kwa sisi, tuipende nchi yetu, tujenge umoja na mshikamano na wote tufanye kazi kwa bidii na maarifa kwani maisha bora hayatadondoka kama mana katika Jangwa la Sinai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaelekea kwenye Uchaguzi, wengi wenu hapa mnaingia kwenye kinyag'anyiro, nataka niwatakie kila la kheri. Nami mnitakie kheri na mgombea mwenza wangu Dr. Mohamed Ghalib Bilal ambaye ninaamini tutasaidiana vizuri kupeperusha bendera ya CCM katika kampeni ya kukitafutia chama chetu ushindi mnono

kama safari ile au hata kuzidi wakati ule ili tukutane tena Bunge lijalo na kipindi kijacho kwa sasa wananchi ndiyo wakati wao wa kuamua. Sisi katika Serikali tumejiandaa na vyombo vyote husika vimejiandaa kwa uchaguzi huu kuwa wa amani, huru na wa haki kama ilivyo sifa ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa kunisikiliza. Mungu Ibariki Afrika, Mungu Ibariki Tanzania. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Rais. Sasa Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Wageni waalikwa, tusimame kwa ajili ya Wimbo wa Taifa.

WIMBO WA TAIFA

(Hapa Wimbo wa Taifa Uliimbwa na Waheshimiwa Wabunge)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, shughuli zote za Bunge la Tisa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zimefikia hatma yake, sasa ni mwisho. Kwa hiyo, naliahirisha Bunge hadi hapo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano atakapoliita tena. *(Makofi)*

WABUNGE FULANI: Hutoi hoja?

SPIKA: Aah, hii ni dhahiri, hamuwezi kubaki hapa! *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyopo mbele yetu ni kuliahirisha Bunge hadi hapo litakapoitwa tena na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Hoja ya Kuahirisha Bunge mpaka litakapoitishwa tena na Rais ilipitishwa na Bunge)

SPIKA: Kwa masikio ya Mheshimiwa Spika, walioafiki wameshinda na wasioafiki ni waoga. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa naliahirisha Bunge hadi hapo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atakapoliita rasmi.

(Saa 12.20 jioni Bunge lilifungwa mpaka Siku litakapoitishwa tena na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)